# ADILI NA NDUGUZE



SHAABAN ROBERT

Kwa

Marafiki wazawa wa Afrika

Pamoja na wazungu wapenda Afrika

YALIYOMO


Utangulizi

Wahusika katika hadithi

Mfalme Rai

Siri inafichuka

Adili mbele ya Rai

Ndugu zake

Mgao mwingine

Tandu na nyoka

Mji wa mawe

Mrithi wa mji wa mawe

Mji ulivyogeuka mawe

Kutoswa kwa Adili

Wokovu wa Adili

Nduguze kuwa manyani

Adhabu ya kwanza

Kula na manyani

Arusi

# UTANGULIZI

Ingawa kitabu hiki hutaja habari za malaika na majini, na viumbe wa ajabu, lakini ni kwa sababu ya utunzi tu. Mambo hasa yaliyotiliwa mkazo ndani yake ni ardhi na mimea yake; machimbo na hazina zake; mifugo na mazao yake; biashara na faida yake; safari na manufaa yake; utajiri na baraka yake; ahali na heshima zao; na ndugu na matendo yao. Mambo haya huhusu watu wengi kama si dunia nzima. Kwa kuwa yahusu maisha mbalimbali, yatazamiwa kuwa kitabu chenyewe hakitakosa kupendeza wasomaji wake. Jitihada ya kuepuka karaha imefanywa, lakini mikasa inayotokea kwa baadhi ya wanadamu imesimuliwa kinaganaga katika kila sura.

SHAABAN ROBERT

January, 1951

## WAHUSIKA KATIKA HADITHI

1. Rai
   Mfalme mwadilifu wa Ughaibu

2. Maarifa
   Waziri mkuu

3. Ikibali
   Mshauri na mshairi

4. Adili
   Liwali bora wa Janibu

5. Faraja
   Baba yake Adili

6. Hasidi
   Ndugu wa kwanza wa Adili aliyekuwa hasidi

7. Mwivu
   Ndugu wa pili wa Adili mwenye wivu

8. Mwelekevu
   Binti mfalme na mrithi wa mji wa mawe

9. Tukufu
   Mfalme wa mji wa mawe

10. Enzi
    Malkia wa mji wa mawe

11. Mrefu
    Jitu la ajabu

12. Kabwere
    Mganga

13. Huria
    Binti mfalme wa majini

14. Kisasi
    Mfalme wa majini

15. Mjeledi
    Malkia wa majini

16. Hunde
    Waziri wa ngazi na kiumbe mbaya kabisa

# MFALME RAI

Rai, mfalme wa Ughaibu, alikuwa mfalme wa namna ya pekee duniani. Alikuwa na tabia iliyohitilafiana kabisa na tabia za watu wengine wa zamani zake. Tabia yake ilijigawa katika theluthi tatu mbalimbali kama za rangi ya ngozi ya pundamilia.

Kwa theluthi ya kwanza alikuwa msuluhishi akipendwa na watu, kwa theluthi ya pili alifanana na Daudi akiheshimiwa kama mtunzaji mkuu wa wanyama, kwa theluthi ya tatu alikuwa kama Sulemani akatiiwa na majini.

Kutawala suluhu na mapenzi ya wanadamu, utunzaji wa wanyama, na utii juu ya viumbe wasioonekana kama majini hutaka uwezo mkubwa sana. Kwa hivi, fikiri wewe mwenyewe jinsi Rai alivyojipambanua mwenyewe na wafalme wengine.

Katika miliki ya mfalme huyu kodi ilitozwa juu ya mifugo ya wanyama. Kodi hii ilihalalishwa kwa sababu Ughaibu ilikuwa nchi ya mifugo. Ughaibu ilipokuwa juu ya kilele cha ustawi, mifugo yake ilikuwa hailingani kwa ubora na mifugo ya nchi yoyote nyengine ulimwenguni.

Fahari yake ya mifugo ilikuwa kubwa kabisa. Fahari hiyo haikuwezekana kukaidika ikitazamwa kwa wivu katika dunia nzima. Malipo ya kodi hii yalifanywa kwa wanyama waliozaliwa pacha. Kila zizi lilitozwa pacha moja kila mwaka.

Mazizi yaliyokuwa hayana wanyama waliozaliwa pacha katika mwaka uliodaiwa kodi yalisamehewa. Zizi lililoshindwa kulipa kodi lilitokea kwa nadra sana kwasababu mifugo yote ilikuwa mizazi ya ajabu. Zilipatikana pacha katika mbuzi, kondoo, ng'ombe, farasi na wanyama wengine.

Masurufu ya serikali ya Ughaibu yalitegemea juu ya wanyama wake. Kwa sababu hiyo kila zizi katika nchi hii lilihesabiwa kama hazina maalum, na kila mnyama wa zizi hilo alikuwa kama johori hasa. Mazizi yaliyopotelewa na mifugo yake kwa maradhi yalijazwa tena wanyama wapya. Maskini waliotaka mifugo, lakini waliokuwa hawana njia ya kuipata, walikabidhiwa

haja zao na serikali bila malipo yoyote. Basi mifugo ilienea katika nchi yote ya Ughaibu.

Kwa masurufu haya na misaada kama hii , uangalifu wa mfalme juu ya wanyama wa mifugo ulikuwa hauna kiasi wala kadiri, huruma yake juu ya wanyama wasiokuwa wa mifugo ilishawishika sana.

Rai alikuwa kiongozi muadilifu na mfalme mwema sana. Hakusita kufanya kazi ndogo wala kubwa kwa mikono yake mwenyewe. Zile ambazo hakuwahi kuzitenda yeye mwenyewe alipenda kuziona kwa macho yake zikifanywa. Kwa bidii zake kubwa aliweza kushiriki katika mambo mengi ya maisha akasaidia maendeleo makubwa ya nchi yake.

Hakulazimisha mtu yeyote kutenda tendo fulani, lakini alishawishi kila moyo wa mtu kuiga alivyotenda kwa hiyari yake mwenyewe. Alikuwa na mvuto mkubwa juu ya mioyo ya watu. Alitumia mvuto huu juu ya watu mpaka nchi yake ilikuwa haina mvivu, goigoi wala mwoga. Kuondoa uvivu, ugoigoi na woga katika nchi ni kazi ngumu.

Mambo haya yanapendwa sana na watu ingawa yana madhara makubwa kwao. Kwa hivi, kufaulu kwa Rai kulistahili sifa kubwa sana. Sifa yake ilifurahiwa na viumbe wote.

Malaika mbinguni waliitungia mashairi; ndege hewani waliiimba kwa sauti zao nzuri; wanadamu duniani waliisimulia kwa hadithi; majini na mashetani waliikariri kwa tenzi. Rai alikuwa mtu mmoja kati ka watu bora waliopata kutoka tumboni mwa mwanamke. Alifanya urafiki na viumbe mbalimbali kwa sababu aliwajali wote.

Ilikuwa ni desturi ya Rai kusema maneno na kuacha watu wengine watende matendo, lakini alifanya matendo na akaacha wengine waseme maneno. Tendo hukidhi haja maridhawa kuliko neno. Haja ikishughulikiwa kwa matendo hupatikana upesi,lakini ikishughulikiwa kwa maneno huchelewa kama sadaka.

Rai alifahamu haya lakini watu wake hawakufahamu. Hawa walipaswa kuamshwa katika usingizi wao kwa matendo, siyo kwa maneno. Maisha ya Rai yalipita matendo mbalimbali.

Katika hukumu alikuwa imara sana. Hakupendelea mkubwa wala hakumdhulumu mdogo. Watu wote walikuwa sawasawa mbele ya sheria. Hakuuza haki za watu kwa rushwa. Wanadamu na wanyama walipata haki zao katika baraza lake. Hili ndilo tendo moja katika matendo yake ambalo limetia jina lake katika makumbusho yasiyosahaulika katika wakati wake, sasa na baadaye katika wakati ujao duniani.

Kila mtu alipoiga matendo ya mfalme yabisi katika nchi alifukuzwa. Rutuba ilienea kila mahali. Kwa rutuba hii ardhi ya Ughaibu ilikuwa na rangi ya kahawia. Juu ya ardhi hii paliota mimea iliyofanana na zabarijudi kwa uzuri. Mimea hii ilieneza neema ya vyakula kwa watu na malisho ya wanyama. Hewa ya nchi nzima ilinukia manukato kwa maua mazuri ya mimea mbalimbali.

Siku moja mfalme Rai alipokuwa akitizama hesabu za wanyama waliokusanywa kwa kodi , aliona karibu mazizi yote katika milki yake yamekwisha lipa kodi zake ila mazizi ya Janibu. Ugunduzi huu uliamsha wasiwasi mkubwa uliokuwa ukingojea mguso mdogo tu katika moyo wake.

Moyo wake ulipokuwa ukiliwa na wasiwasi, mawazo mbalimbali yalipita katika akili yake. Alidhani kuwa labda Janibu imepatwa na mwaka wa kiu, na kuwa malisho ya wanyama yameharibika.

Labda sotoka imeshambulia mazizi katika nchi, na kuwa vifo vingi vimetokea katika mifugo. Kwa kuwa wanadamu na wanyama wana shirika moja katika maisha, Rai alihamadika sana. Aliona dhahiri kuwa madhara ya wanyama ni hatari kwa watu vilevile.

Rai alikuwa na akili tambuzi iliyopenya katika mashaka mengi ya maisha. Walakini, hizi zilikuwa dhana tu. Dhana zenyewe zilikuwa haziwezi kusaidia kujibu ugunduzi wake. Palikuwa hapana kitu kilichoweza kuthibitisha.

Ughaibu na Janibu ilikuwa miji miwili mbalimbali chini ya milki moja. Miji hii ilitengwa na umbali mkubwa. Ugunduzi wa Rai katika hesabu ya kodi ulisafiri upungufu ambao haukutazamiwa. Sababu ya upungufu ule haikujulikana kwa sababi habari za Janibu zilikosekana.

Pasipo shaka, hukubalika bila ya swali kuwa miji miwili ina ndoto mbili zenye maana mbalimbali. Rai aliweza kujua tafsiri ya ndoto ya Ughaibu kuwa jumla ya kodi ilikuwa nakasoro, lakini hakuweza kujua maana ya ndoto ya Janibu, yaani sababu ya kasoro ile.

Mambo katika maisha yamo katika mwendo huu siku zote. Hayajulikani mpaka yamechunguzwa na kuthibitishwa kwanza. Rai alikuwa mtu arifu wa mwendo huu. Kwa hivi, shauri hili liliachwa kwa Maarifa, waziri mkuu, kuchunguzwa.

SIRI INAFICHUKA

Ikibali alitakiwa na maarifa kwenda Janibu kuchunguza kodi. Ikibali alikuwa mshauri katika halmashauri ya Ughaibu na mshairi wa mfalme. Alichaguliwa kwa kazi hii kwa sababu alikuwa na maarifa ya kuchukuana na watu. Kwa maarifa haya aliweza kupata mradi wake siku zote bila ya kuamsha uadui wa watu juu yake.

Ughaibu ilikuwa teuzi katika wasimamizi wake na katika madaraka yao. Uteuzi wake ulikuwa na maana kwa sababu ukamilifu wa mtu duniani ni tabia njema. Mbali na sifa nyengine, kila mtu bora alitakiwa kuonyesha ubora wake kwa kuchukuana na watu. Ikibali alikuwa mkamilifu wa tabia, akaaminiwa na Rai, Maarifa na watu wadogo.

Siku ya pili, saa moja asubuhi, Ikibali alikwenda Janibu.

Mwendo wa saa sita kwa farasi ulikuwa kati ya Ughaibu na Janibu. Adhuhuri ilipokaribia Ikibali alikuwa amefika katika viunga vya mji aliokusudia. Huko alitua akapeleka taarifa kwa Adili, liwali wa Janibu kuwa amewasili. Adili alipopata habari alikwenda akamlaki mgeni wake nje ya mji kwa furaha.

Baada ya kumlaki aliingia naye mjini. Saa saba mchana Ikibali alifika nyumbani kwa mwenyeji wake akapokewa kwa taadhima. Alikula chakula cha mchana na mudir wa Janibu, saa nane akazuru idara zao, hulka ya Ikibali ilipendeza watu waliopata kukutana naye. Kicheko kilikuwa midomoni mwake na shukrani katika pumzi zake. Hulka njema ni sawa na mali. Fundisho hili linakwenda duniani mpaka sasa.

Jioni Ikibali na Adili walipokuwa peke yao mazungumzo juu ya kodi yalianza. Hapakuonekana upungufu wowote. Hesabu haikuwa kamili tu, lakini ilionyesha ziada vilevile. Ikibali alihakikishiwa kuonyeshwa ziada hii asubuhi.

Sababu ya kuchelewa ilihusisha makusanyo ya ziada.

Kama Adili hakutanguliwa na Ikibali siku moja, Adili alikusudia kupeleka hesabu yake Ughaibu siku ya pili. Ikibali alifikiri habari hizi njema zilitosha kutuliza moyo wa mfalme.

Kwa hivi, aliazimu kurudi Ughaibu kesho yake, Adili alitaka kutajamali na Ikibali. Hamu yake ilikuwa kubwa sana. Kama haja hii haikumkalifu Ikibali, Adili aliomba sana jamala ya kutafaraji naye kwa muda wa siku tatu. Kwa kuwa waungwana hawanyimani neno lisilokalifu Ikibali alikubali kuhairisha marejeo yake.

Sasa Adili na mgeni wake waliingia sebuleni. Sebule hiyo ilikuwa imesakafiwa kwa marmar za rangi tatu, yaani nyeupe, nyekundu na samawati. Dari yake iliikizwa vizuri sana. Ilisaki sawasawa juu ya kuta nne zilizopakwa sherezi ya manjano.

Katikati ya sari hii ilining'inia chini karabai moja iliyozungukwa na matovu ya almasi. Kuta mbili katika hizi nne zilikuwa na madirisha mazuri. Katikati ya sakafu palitandikwa mazulia ya thamani kubwa.

Juu ya mazulia hayo palikuwa na meza moja ya mkangazi na viti viwili vya henzirani.

Vyakula na vinywaji mbalimbali viliandaliwa juu ya meza. Walikaa kitako hapo kwa kuelekeana, wakala chakula cha usiku. Baada ya kula na kunywa waliongea mpaka wakati wa kulala.

Malazi ya Ikibali yalifanywa katika chumba kilichokuwa na marmar nyeupe tupu. Dari ilipakwa sherezi ya samawati na kuta zilikuwa na sherezi ya zari. Kila ukuta ulikuwa na dirisha la kioo kilichosimama juu ya mihimili ya johari.

Vitanda viwili vya pembe vilivyokuwa na viwambo vya ngozi na matandiko ya pamba vilitandikwa humo. Mihimili ya vyandarua ilikuwa ya dhahabu. Siku ile Adili alilala katika chumba kimoja na mgeni wake. Baada ya kupanda vitandani wote wawili walinyamaza kimya.

Kila mtu alidhani mwenzake amelala, lakini wote wawili walikuwa macho. Ikibali alikuwa akisanifu mashairi, kama ilivyokwisha semwa, alikuwa

mshairi mashuhuri.

Alipoendelea hivyo mpaka usiku wa manane alimuona Adili ameondoka ghafla kitandani. Chumbani lilikuwemo bweta. Adili alipokwisha vaa nguo zake aliliendea bweta akalifungua. Alitoa mjeledi na mshumaa.

Mshumaa ulipowashwa nuru kubwa sana ilitokea. SasaAdili alifungua mlango wa chumbani akatoka nje. Hakujua kwamba Ikibali alikuwa macho.

Ikibali alishangaa, usanifu wake ukachafuka. Hakujua Adili alikusudia kwenda wapi na mjeledi usiku ule. Alijua kwamba si murua kunyemelea mambo ya watu, lakini alijua pia kwamba alikuwa na wajibu kujiweka tayari kusaidia katika haki.

Kwa sababu ya msaada aliona haifai kulala kama mvivu nafasi ya kutenda wajibu wake ilipotokea. Wazo hili lilimuondoa kitandani akatoka nje. Alimfuata Adili nyuma polepole.

Karibu ya nyumba moja ndogo Ikibali alisimama kando. Adili alifululiza mpaka mlangoni. Aliufungua akaingia ndani. Alipotoka nje alikuwa na sinia moja. Siniani mlikuwa na sahani za chakula na birika la maji. Alijibandika begani sinia akaenda zake.

Ikibali alimfuata nyuma vilevile. Adili alipofika nyumba nyingine, kubwa kuliko ya kwanza, alifungua mlango akaingia ndani. Nyuma yake mlango ulifungwa kwa nguvu. Ikibali alinyata mpaka mlangoni, akasimama kimya.

Alichungulia ndani katika ufa wa mlango akaona ukumbi.

Katikati ya ukumbi palikuwa na kitanda kizuri na meza moja. Manyani mawili yaliyofungwa viunoni minyororo ya dhahabu yalikuwa yamelala kitandani. Adili aliweka sinia juu ya meza . Nyani moja lilipofunguliwa likalialia kinyonge.

Adili alilikamata akalifunga miguu ya mbele na nyuma kwa kamba. Alipolitupa chini alishika mjeledi kwa mkono wa kulia akalipiga mpaka likazirai. Nyani lingine lilipigwa mpaka likazirai vilevile. Manyani

yalipozinduka yalinasihiwa. Adili aliapa kuwa hakufurahi kuyaadhibu, na kwamba alitazamia faraja yao kutokea karibu.

Sasa manyani yalichukuliwa mezani kula chakula kwa vijiko na nyuma. Yaliposhiba yalinyweshwa maji. Midomo yao ilifutwa kwa leso za hariri. Mambo haya yalipotendeka Ikibali alikuwa amesimama kimya anachungulia.

Adili alipokusanya vyombo ili atoke nje , Ikibali alitangulia kuondoka mlangoni. Alikwenda mpaka kitandani pake akajilaza kimya kama aliyekuwa hajui lililotokea. Kitambo kidogo Adili alirudi akaweka mjeledi na mshumaa bwetani.

Hakushuku neno, na baada ya kuvua nguo zake alilala tena.

Lakini tangu wakati ule mpaka asubuhi, Ikibali hakupata usingizi kwa mawazo mbalimbali. Kila njia ya fikira aliyokwenda haikumfikisha katika tafsiri ya mwujiza ule. Adili alikuwa mtu wa maana. Hakutazamiwa kufanya ukatili kwa wanyama.

Mwenyeji na mgeni waliondoka vitandani. Baada ya kuoga na kuvaa walikwenda sebuleni kustaftahi. Walipokwisha walikwenda mazizini kutazama wanyama waliokusanywa. Siku ile moyo wa Ikibali ulikuwa mzito kwa mawazo, lakini hakuuliza neno juu ya siri aliyogundua. Ilikaa moyoni mwake mwenyewe.

Siku ya pili, usiku wa manane vilevile, Adili alifanya tena aliyofanya jana. Siku ya tatu mambo yalikuwa yaleyale. Katika muda huu wote ikibali hakuacha hata siku moja kumfuata na kutazama matendo yake. Siku ya nne alipewa hesabu aliyojia na kurudi Ughaibu. Kwa kesha ya siku tatu hakuwza kuongoza vyema farasi kwa usingizi. Laiti asingekuwa na uzoefu wa kupanda farasi angalitupwa chini njiani amelala.

Alipofika Ughaibu alitoa ujumbe wake. Alitaka sana kuficha siri ya manyani ya Adili na adhabu yao, lakini hakuweza. Alifikiri kama Adili aliyaadhibu kwa ukatili tu asingelijisumbua kuyafuga, kuyalisha na kuyanasihi. Mtu hawezi kutunza kitu asichojali. Zaidi ya umahiri, werevu na usuluhifu, Ikibali aliweza kufahamu upande wa pili wa neno.

Aliona dhahiri kuwa Adili hakupenda adhabu ile kuendelea. Kama aliitenda kwa kulazimishwa alikuwa na haki ya kusaidiwa. Yamkini mfalme aliweza kumsaidia. Kwasababu hii alitoa siri aliyokuwa nayo. Rai, aliposikia nywele zake zilisimama kichwani, na damu yake ikasisimka mwilini. Ikibali alitumwa tena Janibu kumleta Adili na manyani mbele ya mfalme.

# ADILI MBELE YA RAI

Uso wa Ikibali ulikuwa na haya na moyo wake ulijaa hisani. Alikuwa tayari kutumika kama alivyotakiwa na mfalme, lakini alichelea kuwa haini kama siri aliyotoa ilikuwa maangamizi kwa Adili. Alijuta ulimi wake haukuwa na nadhari. Hapana roho mbinguni wala duniani isiyopatwa na majuto.

Tuna busara nyingi sana baada kuliko kabla ya neno kufanyika. Kama taratibu ya msaada haikufaulu, Ikibali hakupenda kumkabili Adili. Wakati ule ule hakuweza kughairi dhima yake . Ugomvi baina ya hiari na dhima ulianza moyoni mwake. Mambo haya mawili hayatimiziki mara moja. Hapana mtu awezaye kwenda njia mbili kwa wakati mmoja. Kwa hivi, Ikibali alitii mahitaji ya dhima yake akaenda Janibu.

Adili alipoona Ikibali amerudi, alishtuka. Alisema moyoni mwake ataokolewa katika uovu aliolazimishwa kuutenda lakini hakupenda kuutenda. Baada ya hapo alimuuliza Ikibali neno lililomrudisha ghafla Janibu. Ikibali alijibu asingelirudi ghafula vile, lakini katika jitihada yake ya kutenda wema ametenda nuksani.

Alikuwa hana udhuru wa kujitetea katika lawama lake. Ulimi wake mwenyewe umemponza. Aliungama kuwa, alipofika Janibu mara ya kwanza alishawishika kumpeleleza Adili siku tatu. Kila usiku alipokwenda kuadhibu manyani, yeye alimfuata nyuma.

Aliporudi nyumbani kulala, yeye alitangulua mbele. Mambo yaliyotendeka kwa manyani yalikuwa ajabu kwake. Hakupata kuuliza sababu yake. Aliporejea Ughaibu alizungumza habari zile kwa mfalme. Mfalme aliposikia alimrudisha Janibu kumchukua Adili na manyani wake.

Adili alikuwa mwema na msamehevu. Alikubali kama Ikibali alilaumika kwa kutoa siri, kadhalika yeye mwenyewe alilaumika kwa ukatili. Tafakuri ilimuonyesha Adili kuwa ukali wa mbwa hutokana na msasi. Mbwa wa msasi mkali ni wakali pia. Rai alikuwa mfalme muadilifu.

Alijuzu Ikibali, mjumbe wake, kuwa mchunguzi hodari. Mambo yalipogunduliwa yalikuwa kweli.

Mambo yenyewe hayakumpendeza Adili mwenyewe, licha ya mfalme na mjumbe wake. Kipawa kimoja katika vipawa bora kwa mwanadamu ni ujuzi wa maovu. Adili alibarikiwa kipawa hiki.

Alishukuru kuwa siri iliyogunduliwa imefika katika masikio ya mfalme. Adili mwenyewe alitaka ijulikane, lakini alichelea kuwa haini kwa mfadhili wake. Madhali imefichuka alikuwa tayari kuithibitisha. Adili alijiandaa kwa safari ya mwito wa mfalme. Farasi watatu walitandikwa matandiko mazuri. Yeye alipanda farasi mmoja na mmoja kwa kila nyani. Ikibali alipanda farasi wake mwenyewe. Farasi wa Adili na yule wa Ikibali walikwenda sambamba njiani.

Nyuma yao waliandamana manyani juu ta farasi. Kila mtu aliyeyaona manyani yamepanda farasi alistaajabu. Mnyama kupanda juu ya mnyama ilikuwa upeo wa miujiza kwa watu. Vinywa vya umati wa watu vilikuwa wazi kwa kivumo cha lo salala! Wakati umefika wa mawe kusema, miti kujibu na wanyama kuwa watu.

Ikibali aligeuza uso wake kwa Adili akasema kwa ucheshi. “Mbwa wanatubwekea kama walionusa mtaro wa windo”. Adili alikubali kwa kuinamisha kichwa na kutabasamu, walisafiri hivi mpaka Ughaibu. Baada ya kutua Adili alipelekwa mbele ya mfalme na manyani yake.

Manyani yalipomuona mfalme walifanya ishara mbili. Kwanza yaliinua juu mikono yao kama yaliyokuwa yakiomba, pili yalilialia kama yaliyodhulumiwa. Ishara ya kwanza ilionyesha ombi la msaada, na ile ya pili ilionyesha mashtaka. Licha ya Rai, hata mimi na wewe tungelitafsiri hivi kama tungelikuwa katika baraza hilo.

Mfalme alipooona vile alitaka kujua kwa Adili sababu ya kuadhibiwa, kulishwa na kunasihiwa manyani yale kila siku. Katika sababu zake alionywa kusema kweli tu. Adili alijibu kuwa waungwana hawasemi uongo. Atasema kweli, na manyani yatakuwa mashahidi. Maneno yake yakiwa uongo, yatakanushwa na manyani kwa mguno, lakini yakiwa kweli, manyani

yatathibitisha kwa kuziba nyuso zao kwa viganja vya mikono yao. Sasa kisa baada ya kisa juu ya manyani kikasimuliwa.

NDUGU ZAKE

Katika kisa cha kwanza Adili alisema manyani yale ni ndugu zake. Baba yao alikuwa mmoja na mama yao mmoja. Baba yao aliitwa Faraja. Faraja alikuwa mtoto wa pacha. Wakati wa kuzaliwa pacha hao, mmoja alikufa pakabaki mmoja. Huyu aliyebaki aliitwa faraja kwasababu aliwafariji wazazi wake katika msiba wa ndugu yake. Alipokua wazazi wake walimuoza mke, yaani mama yao.

Mama yao alichukua mimba ya kwanza akazaa mwana aliyeitwa Hasidi. Alichukua mimba ya pili vilevile akazaa mwana aliyeitwa Mwivu. Alichukua mimba ya tatu akazaa mwana tena aliyeitwa Adili. Walilelewa mpaka wakawa watu wazima wenye vichwa vilivyofunzwa lakini mioyo isiyosahauliwa. Busara kubwa kichwani haina faida kama moyoni hamna chembe ya wema.

Baba yao alipokufa aliacha shamba zuri, duka kubwa, mifugo mbalimbali na nakidi shililingi hamsini elfu. Walimzika kama desturi na kufanya matanga. Siku arobaini zilipopita, Adili alikaribisha matajiri na watu maarufu wa Janibu karamuni. Karamu ilipokwisha Adili alitamka kuwa maisha ni safari, dunia ni matembezi kwa mwanadamu. Maskani yao ya milele yapo peponi. Hapana mtu ambaye atabaki duniani. Baba yake amekufa akiacha mali nyingi.

Alichelea kuwa walikuwako watu waliomdai au walioweka dhamana kwake. Alitaka kila mtu apate kulipwa ili aondoe lawama la baba yake ulimwenguni. Baada ya kusema hivyo kimya kikubwa kilitokea. Watu walinyamaza kama waliokuwa wamenyang’anywa ndimi zao.

Halafu walijibu kwa umoja kuwa hawakuweza kuuza pepo kwa dunia. Walikuwa wacha Mungu na wafuasi wa haki.

Walifahamu halali na haramu. Jambo moja katika waliyokimbia kabisa lilikuwa mali ya yatima. Walimfahamisha Adili kuwa mali ya baba yake ilikuwa imebaki mikononi mwa watu. Bila shaka watu hao watamlipa.

Hapakuwa na mtu hata mmoja miongoni mwao aliyedai kitu kwa marehemu. Walithibitisha kuwa walimsikia mara nyingi baba yake Adili akisema kuwa

alichelea sana deni. Katika uhai wake alizoea kuomba asife na deni.

Tabia ya baba yake ilikuwa kamili. Kila karadha aliyochukua alilipa kabla ya kudaiwa. Alipokopesha kitu kwa mtu hakudai kwa fadhaa. Wadeni wake walimlipa polepole. Mtu aliyekuwa hana njia ya kulipia alisamehewa.

Adili aliwashukuru kwa kuhudhuria karamuni na kwa kumpa hakika ya ukamilifu wa baba yake. Wageni walipokuwa wanakwenda zao waliambiana njiani.

” Mwana wa mhunzi asiposana huvukuta. Adili alikuwa mwema kama baba yake”.

Sasa Adili aliwaambia ndugu zake kuwa, kwa ushahidi uliotolewa, alitosheka kuwa baba yake alikuwa hadaiwi na mtu. Urithi walioachiwa ulikuwa mkubwa sana.

Warithi walikuwa watoto watatu tu. Aliuliza ndugu zake, walipenda urithi ule ugawiwe kila mtu achukue sehemu yake, au uachwe kama ulivyokuwa ili watumie shirika. Ndugu zake walitaka urithi ugawiwe kati yao.

Adili alikwenda kumwita kadhi. Kadhi alipokuja aligawa urithi wao katika mafungu matatu. Mafungu yote yalikuwa sawasawa kwa thamani. Kila mtu alipata fungu lake. Adili, alichukua shamba na duka. Mali nyingine walipewa ndugu zake.

Basi adili alifungua duka lake.

Alinunua bidhaa akatia dukani mpaka likajaa tele. Alikaa kitako akafanya biashara. Ndugu zake walinunua marobota ya ngozi na bidhaa nyengine wakafanya safari ya kwenda nchi ngeni kufanya biashara

Siku ya kuagana nao, Adili aliomba Mungu awabariki ndugu zake ugenini, naye ampe riziki yake kwao. Alifanya biashara kwa muda wa mwaka mmoja. Hakuacha kuhesabu kitu alichonunua wala alichouza.

Vitu vyote, kilichoingia ndani na kilichotoka nje, vilitiwa daftarini kwa uangalifu. Mali bila daftari hupotea bila habari. Adili alikuwa macho sana

juu ya neno hili. Aliweka hesabu ya kila siku na ya kila mwezi. Mwisho wa mwaka alipolinganisha faida na hasara aliona amepata mali kama ile iliyoachwa na baba yake. Hakika mtu anayehesabu mapato na matumizi hafi maskini.

Siku moja Adili alikuwa amekaa dukani pake. Ulikuwa wakati wa baridi. Alikuwa amejifunika mablanketi mawili. Moja lilikuwa la sufu na jingine la pamba. Aliona ghafla watu wawili wanakuja dukani. Walikuwa hawana kitu. Kila mmoja alivaa kanzu mbovu bila ya nguo nyengine ndani. Midomo yao ilibabuka kwa baridi.

Alipotambua kuwa walikuwa ndugu zake, moyo wake uliwaka moto kwa huzuni. Watu aliowapenda walikuwa katika hali mbaya sana. Aliondoka kitini akaenda kuwakumbatia. Mitiririko wa machozi ya moto ilitoka machoni mwake. Hakuweza kujizuia kulia kwasababu ya mapenzi makubwa aliyonayo juu ya ndugu zake. Mapenzi yake yalitoneshwa na hali mbaya waliyokuwa nayo.

Adili alikuwa tayari siku zote kugawana na mtu yeyote tonge moja la chakula lililokuwa mkononi mwake. Alipoona ndugu zake katika matambaa hakuweza kuhimili. Uchi wao ulikuwa uchi wake. Alivua mablanketi yake mwenyewe akampa kila mmoja lake. Maji ya moto yalitengenezwa, akawapeleka msalani kuoga.

Kisha alitoa sandukuni vikoi viwili, fulana mbili, kanzu mbili, jozi mbili za viatu na kofia mbili akawapa.

Vitu hivyo vilikuwa vizuri na thamani yake ilikuwa kubwa sana.

Baada ya kuvaa nguo, walikaribishwa sebuleni. Wakati ule hali yao ilikuwa bado dhaifu sana kwa uchovu na njaa. Chakula kililetwa katika sinia moja ya dhahabu iliyonakshiwa kwa fusifusi.

Walitafadhaliwa kula chakula, wakala mpaka wakashiba. Adili aliyageukia manyani akauliza kama yaliyosemwa yalitokea au hayakutokea. Manyani yaliziba nyuso kwa viganja vya mikono yao kwa aibu.

MGAO MWINGINE

Katika kuelezea msiba wao, ndugu zake Adili walisema walipoondoka Janibu walikwenda Gube. Walianza kuuza bidhaa zao huko. Ngozi iliyonunuliwa Janibu kwa shilingi moja iliuzwa kwa shilingi kumi, na ile ya shilingi mbili kwa shilingi ishirini.

Walipata faida kubwa sana. Baadaye walinunua viatu kwa bei ya shilingi kumi jozi moja . Viatu hivyo vingalifika Janibu vingaliuzwa kwa shilingi arobaini kila jozi. Walipotoka Gube walikwenda mji wa Gharibu wakafanya biashara kubwa kuliko mara ya kwanza. Walishindwa kujua heaabu ya fedha waliyoipata, walisifu uzuri wa miji waliyokwenda, usitawi wa biashara na faida iliyopatikana huko.

Mtu kushindwa kujua pato lake mwenyewe huonyesha uchache wa uangalifu. Lakini Adili hakusema neno juu ya hili. Ulikuwa si wakati wa kusema makosa. Ndugu zake walitaka huruma wakati ule na siyo kulaumiwa.

Kisha waliendelea kusema msiba wao ulikuwa hausemeki. Walipoona wamepata mali nyingi hawakufurahi kukaa ugenini tena. Iliwatokea dhahiri kuwa mtu huchuma juani akala kivulini na ugenini ni juani. Fikira hii ilipowatopea walifanya safari kurudi kwao.

Basi walijipakia chomboni. Kwa muda wa siku tatu safari yao ilikuwa njema, lakini siku ya nne bahari ilichafuka. Mvua ilianza na giza lisilopenywa na nuru lilifunika bahari. Mchana ulikuwa kama usiku. Palitokea radi na umeme. Dhoruba kali iliandama nyuma. Mawimbi makubwa kama mlima katika bahari isiyopimika kina yaliwakabili. Jahazi yao ilipeperushwa kama jani mwambani ikavunjika.

Shehena ya mali ilikuwa chomboni ilitota. Fikira ya mali yao haikuwajia, waliomba wokovu wa maisha yao tu. Kwa msaada wa mbao chache zilizopatilana katika chombo kilichovunjika, walielea baharini mchana na usiku kwa muda wa siku sita.

Siku ya saba, walipokuwa karibu kukata tamaa, jahazi ilipita karibu, mabaharia wa jahazi hiyo waliwaokoa. Jahazi iliyowaokoa ilikuwa na safari

ya kwenda nchi nyingine. Iliwapasa kuwa katika safari ile na kufanya kazi bila ujira chomboni. Waliposhuka katika kila bandari waliyofika waliomba chakula. Katika baadhi ya miji walipewa chakula, lakini katika miji mingine hawakupata kitu.

Kwa hivi, waliuza nguo walizovaa wapate fedha ya kununulia chakula. Uchi wao uliweza kungojea nguo, lakini njaa yao haikuweza kungoja chakula, walipata robo tatu za mashaka ya dunia toka siku waliyokufa maji mpaka siku waliyofika kwao. Laiti wasingalipatwa na bahati mbaya wangalirudi Janibu na utajiri mkubwa.

Ndugu zake walikuwa masogora katila kusema. Walijifunza sana kutumia ulimi na midomo. Adili alivutwa na maneno yao siku zote. Hakujua kama tumaini lake juu ya ndugu zake lilikuwa kazi bure. Walikuwa waovu katika kila inchi ya miili yao. Baada ya kuwasikiliza aliwapa pole. Alisema kuwa mali hufidia roho, lakini roho haifidiwi na kitu.

Salama ya maisha yao ilikuwa bora kuliko faida iliyopotea. Umaskini umetengana hatua moja tu na utajiri.

Kwa kuwa vitu hivi vimekaribiana sana, wako watu katika dunia waliopata kuonja uchungu wa umaskini na ladha ya utajiri. Madhali ndugu zake wameonja uchungu wa umaskini, aliwakuza moyo kutazamia ladha ya utajiri wakati ujao.

Siku ya pili Adili aliwachukua ndugu zake kwa kadhi. Alipofika aliomba mali yake igawanywe mafungu matatu sawasawa kati yao. Alifanya hivyo kwa kuwaambia mali ile pia ilitokana na baba yao. Kila mtu alichukua fungu lake akafungua duka.

Adili aliomba dua kuwa ndugu zake na yeye, wote wabarikiwe. Aliwaonya wenziwe hatari ya uvivu na hasara ya ulevi. Aliwapa chakula na haja nyingine za lazima bure siku zote. Walikaa nyumbani mwake raha mustarehe. Mara kwa mara walipokuwa pamoja, Adili aliambiwa sifa za nchi ngeni. Ndugu zake walikumbuka mali yao na usitawi wa biashara walioona.

Walimvuta Adili kusafiri pamoja nao tena kwa sababu faida za safari, yaani, kufarijika katika hamu, kujua namna ya kuendesha maisha kupata elimu mpya,

kuelewa tabia za watu mbalimbali, kukutana na marafiki wa kweli kushinda ndugu, na mtu mwenye bahati mbaya kwao huweza kupata bahati njema ugenini. Adili aliyageukia manyani akauliza yaliyosemwa yalitokea au hayakutokea. Manyani yaliziba nyuso zao kwa viganja vya mikono kwa aibu.

TANDU NA NYOKA

Moyo hauhimili mshawasha wa mfululizo. Hasa mshawasha wenyewe ukitokana na mtu unayempenda au tamaa ya utajiri. Moyo wa Adili ulikuwa na mapenzi makubwa juu ya ndugu zake. Aliwapenda kama pumzi ya maisha yake mwenyewe. Aliposikia maneno yao alisema haikuwezekana katika maisha yake kukataa haja iliyotakiwa na ndugu zake. Alikubali kusafiri pamoja nao walikopenda.

Fedha ya kuchanga kwaajili ya safari iliyokusudiwa ilikisiwa. Mafungu matatu sawasawa yalitakiwa. Fungu la kila mmoja lilipokusanywa, jumla kubwa sana ya fedha ilipatikana. Walinunua ngozi na bidhaa nyengine. Halafu walikwenda bandarini wakaajiri jahazi kubwa. Walipakia mali yao na vyakula mbalimbali. Siku ya pili walijipakia chomboni wakasafiri.

Adili alisumbuka safari kwa sababu ilikuwa mara yake ya kwanza kusafiri. Baada ya safari ya siku tatu walifika bandarini. Bandari ya kwanza kati ya bandari walizokusudia kwenda. Walishuka wakafanya biashara

Kwa faida iliyopatikana pale, Adili alisadiki maneno yaliyosemwa na ndugu zake.

Waliondoka pale wakaenda mji wa pili. Huko walifanya biashara vilevile wakapata tija kubwa kuliko kwanza. Walikwenda mji wa tatu wakauza bidhaa zao kwa faida kubwa pia. Kabla ya kufika miji yote waliyokusudia kwenda, waliona wamekwisha kurejesha thamani ya mali yao, na faida iliyopatikana ilikuwa kubwa sana. Nusu moja ya mali waliyokuwa nayo ilikuwa imeuzwa. Palibaki nusu ya pili kuuzwa. Walikwenda miji mingine.

Baada ya safari ya siku moja walifika jabalini. Nahodha aliamuru kutua tanga na kutia nanga. Kisha mabaharia walitakiwa washuke jabalini kutafuta maji kwa sababu jahazini mlikuwa hamna maji hata tone moja. Pipa la maji jahazini lililotosha kwa mwezi mmoja lilitoboka. Maji yalivuja bila kujulikana na mtu.

Mabaharia wote walishuka wakatafuta maji chini ya jabali.

Adili alipanda juu ya jabali. Huko aliona tandu linakimbia, rangi yake ya kupendeza sana. Iling'ara kama kioo. Nyuma yake lilifuatwa mbio na nyoka aliyetisha kabisa. Nyoka alipolifikia aliliuma kichwani. Kisha alilibana jiweni. Tandu lilitoa mlio wa kusikitisha. Kwa mlio ule Adili alijua kuwa tandu lilikuwa hatarini. Mara ile moyo wake uliingiwa na huruma. Hakuweza kuvumilia. Aliokota jiwe lililokaribia uzito wa ratili moja akamtupia nyoka. Jiwe lilimpiga nyoka kichwani. Ilikuwa shabaha nzuri sana. Kichwa chote kilipondeka kwa pigo moja akafa mara ile. Ghafula tandu lilijigeuza mwanadamu, yaani msichana mzuri. Uso wake ulivuta macho ya adili kwa haiba yake kubwa. Mbele ya wanawake mia moja wazuri, msichana huyo angalitokea, wote wangalijichukia wenyewe kwa kujiona hawakulingana naye kwa uzuri. Tazamo la mwanaume yeyote lingevutwa kama angalitokewa na msichana huyo. Alikwenda kwa Adili akampa mkono.

Alimshukuru kwa wema aliomtendea. Adili aliombewa dua na msichana apate himaya mbili. Himaya ya duniani na himaya ya ahera.

Ya kwanza imfae katika maisha yake, na ya pili imwokoe siku ambayo mtu hatafaliwa na kitu kingine ila wema aliotenda. Kama alivyookolewa msichana aliahidi kutenda neno lolote jema kwa Adili katika wakati ujao.

Baada ya hayo msichana alielekeza kidole chake cha shahada chini. Mara moja ardhi ilipasuka akaingia ndani yake. Alipokwisha jitia ndani yake, ardhi ikajifunga sawia. Msichana hakuonekana tena. Adili alifahamu kuwa alikuwa si mwanadamu ila ni jini. Kitambo kidogo aliona nyoka aliyemwua akiwaka moto.

Mara moja majivu matupu. Kufumba kope na kufumbua, mahali palipokuwa na jivu palitokea chemichemi ya maji safi. Mambo haya yalikuwa mwujiza mkubwa sana kwa Adili. Alirudi kwa wenziwe na habari za ugunduzi wa maji.

Adili alishangiliwa sana kwa ugunduzi wake. Walipokwisha chota maji ya kutosha walilala.

Asubuhi walitweka wakasafiri mchana na usiku kwa muda wa siku thelathini. Walikuwa hawaoni bara wala kisiwa. Maji yao yalikwisha tena.

Nahodha alipotangaza chomboni kuwa maji yamekwisha mabaharia waliomba chombo kielekezwe upande wa bara.

Lakini nahodha aliapa kuwa hakujua upi ulikuwa upande wa bara toka mahali walipokuwapo. Aliposema hivyo mioyo yao ilihuzunika, machozi yakawatoka machoni njia mbili

Walikuwa hawana neno la kutenda ila kuomba hifadhi ya Mungu. Siku ile walilala na kihoro.

Kulipokucha waliona jabali refu sana baharini. Walianza kufurahi tena. Tanga iligeuzwa wakaenda jabalini. Walipolikaribia walitua. Kisha walishuka chomboni wakapanda jabalini kutafuta maji.

Hali zao zilikuwa dhaifu kwa kiu. Walitafuta huku na huko lakini hawakuona maji. Adili alipanda juu zaidi huko alitazama upande wa pili wa jabali akaona kwa mbali sana kuna ukuta umezunguka.

Kwa kukadiria, ulikuwa ni mwendo wa robo saa toka jabalini mpaka ulikokuwa ukuta. Aliwaita wenziwe waliokuwa chini ya jabali.

Walipokuja aliwaonyesha ukuta alioona. Alidhani ndani yake ulikuwako mji mkubwa ambako maji na vitu vingine viliweza kupatikana. Basi aliwashauri wenzie kwenda kule. Wenzie wote walikataa kwenda. Walichelea kuwa nji wenyewe usije kuwa wa watu wabaya. Wakikamatwa itakuwa mwisho ya maisha yao. Kwa vile walivyokuwa katika hatari ya kiu, hawakuweza kujasiri katika hatari nyingine kwa tamaa ya maji. Walikataa kwenda, wakajitolea wenyewe kufa kwa kiu, lakini Adili hakukubali.

Moyo wake ulikuwa imara sana. Alitaka kujaribu kujiokoa kwanza kabla ya kujitolea kushindwa. Ilikuwa idhilali kwake kujilegeza mbele ya shida iliyowezekana kushindwa. Kwa hivi, alisema kuwa hakuwa na mamlaka juu ya mabaharia wote, lakini alitaka kwenda na ndugu zake. Lo, ndugu zake waliruka, wakakataa kufuatana naye.

Walionywa na Adili kuwa mwanadamu ameumbwa kwa heri na shari, na hasa kwa heri.

Ilikuwa hasara iliyoje kutazama shari tu katika maisha! Juu ya onyo hili ndugu zake hawakuwa tayari kwenda naye. Basi aliwaomba wamngoje jabalini.

Walipokubali kufanya hivyo alikwenda zake peke yake kujaribu bahati yake.

Adili aliyageukia manyani akauliza kama yaliyosemwa yalitokea au hayakutokea. Manyani yaliziba nyuso zao kwa viganja vya mikono kwa aibu.

MJI WA MAWE

Adili alikwenda mpaka ulipokuwa ukuta aliioona. Kimo cha ukuta wenyewe kilikaribia futi arobaini. Juu ulikuwa na upana wa futi kama ishirini. Wote ulikuwa wa mawe yaliyookwa kwa uimara na ustadi.

Mivule, mikangazi, mibuyu na miti mingine ya magogo manene iliota juu yake. Miti yote iligeuka mawe, lakini rangi ya majani yake ilikuwa ya kijani. Maki ya ukuta wote ilikuwa futi ishirini. Duara kubwa sana ilikuwa katikati ya ukuta huo. Katika duara hiyo ulikuwako mji uliokuwa na majengo mazuri sana.

Milango mia moja ilikuwepo ukutani. Milango yote ilikuwa ya chuma kilichokuwa na maki ya futi saba. Ulikuwa mji mzuri na wenye ngome bora duniani.

Milango yake ilikuwa wazi. Adili alipotaka kuingia ndani aliona mtu amesimama mlangoni. Kichwa kikubwa sana cha funguo kilikuwa mikononi mwake. Adili alidhani mtu yule alikuwa bawabu. Alikwenda karibu yake akamwamkia. Hakujibu neno. Alimwamkia mara ya pili na ya tatu lakini hakujibu hata kidogo. Adili alishangazwa na adabu ya mtu aliyemwamkia.

Alidhani hakuelewa lugha yake. Lugha ni pingamizi kubwa kwa watu duniani. Kwa hivi, alimwamkia kwa ishara. Hili liliposhindwa kufaulu alimsogelea akamshika begani. “Bwana umelala nini?” Hakujibu wala hakutikisika. Alizidi kumtazama na kumshika mwilini.

Alipofanya hivyo aliona kwamba alikuwa si mtu ila ni jiwe lililokuwa halina maisha. Ugunduzi huu ulitia mzizimo wa hofu kati moyo wa adili lakini alijikaza. Adili alikuwa si mtu wa kukata tamaa.

Tamaa kwake ilikuwa gurudumu la maisha, naye alijua namna ya kuitawala. Mzizimo wa hofu iliyotamba moyoni mwake uliyeyushwa na udadisi wake mkubwa.

Aliondoka aliposimama na kuingia ndani kidogo. Huko aliona mtu mwingine amesimama barabarani. Alimkaribia akamtazama. Lilikuwa jiwe

vilevile. Alizungukazunguka barabarani. Kila alikokwenda alitazama huku na huko. Mabarabara yote yalijaa watu waliosimama, lakini wote walikuwa mawe matupu. Alipofika sokoni aliona umati mkubwa wa watu. Baadhi yao walikuwa wamekaa kitako na wengine walikuwa wamesimama wima. Mbele ya watu waliokaa palikuwa na vikapu vya nafaka iliyogeuka changarawe, unga uliokuwa vumbi, matunda yaliyobadilika komango, na vitu vingine vya biashara vilivyogeuzwa mawe. Vyote vilikuwa katika hali iliyokuwa haifai kwa chakula. Sababu iliyoweza kueleza mabadiliko yale ilikuwa bado kuonekana. Kwa hivi, Adili aliazimu kuitafuta kwa kila hali. Adili alikuwa na uchunguzi uliomuongoza katika ugunduzi mkubwa.

Alipoondoka sokoni aliona nyumba moja kubwa barabarani. Milango yake ilikuwa wazi. Hili lilikuwa duka la tajiri mkubwa. Alipoingia ndani aliona mwenyewe amelala juu ya kitanda cha dhahabu. Kitanda chenyewe kilitandikwa nguo nzuri na matakia ya zari teule.

Mbele yake palikuwa na kabati lililokuwa na kimo cha futi tano. Tajiri mwenyewe alikuwa mgumu na baridi kama jiwe; na vitu vyake vyote kadhalika. Adili alitazama kabatini akaona mifuko imepangwa safu. Alishika mfuko mmoja lakini kitambaa chake chote kilivumba vumbi.

Vitu vilivyokuwa katika mifuko hiyo ilikuwa sarafu ya dhahabu tupu. Hii haikubadilika mawe wala vumbi

Alijaribu kuchukua dhahabu, lakini hakuweza kama alivyopenda. Moyo wake uliingiwa na fikira kwamba kama angalikuja na ndugu zake wangalichukuwa dhahabu ya kutosha.

Alipotaka kutoka nje aliona makabati yalitiwa nguo za hariri na sufu. Nguo hizo zilikuwa za rangi za mbalimbali na za almaria bora. Aliponyoosha mkono wake kuzishika zilikuwa vumbi kama vitambaa vya mifuko ya dhahabu.

Alitoka akaingia duka jingine. Huko aliona mali nyingi sana kuliko alizoona katika duka la kwanza. Ah, maskini! Mali ilikuwepo lakini haikuwa na wachukuzi. Watu waliokuwa na njaa na jahazi yao iliyokata sheheni walikuwa wamesimama kando kwa zembe. Jahazi ilifika chini ya dafina ya

ajabu, lakini mabaharia wake hawakushuka pwani kupakia. Kula uhondo kwataka matendo. Asie matendo hula uvundo.

Adili alikuwa kama chura kilichofurahia mvua lakini kilikuwa hakina mtungi wa kuwekea maji. Alitamani kuwa na nguvu za ndovu ili achukue dhahabu ya kutosha lakini haikuwezekana. Basi aliingia hapo akatoka. Alikwenda pale akaondoka na fikira ya muujiza alioona.

Kila barabara aliyopita ilikuwa na watu, ng'ombe, farasi, nyumbu, punda na mbwa, lakini wote walikuwa mawe matupu.

Hofu kubwa ilitambaa moyoni mwake kuwa naye asijegeuzwa jiwe. Lakini alijifariji kuwa labda ilikuwako sababu ya mji ule, wanyama na vitu vyake kuwa mawe, na kuwa lile lilikuwa fundisho kwake. Wazo hili lilimpa nguvu, akaendelea kupeleleza.

Alipoingia katika maduka ya masonara aliona wenyewe wamegeuka mawe. Mikino yao ilikuwa imeshika vito vilivyokwisha tengenezwa. Vito vingine vilikuwa ndani ya mikebe. Alipoona vile alitupa mbali dhahabu aliyokuwa nayo kwanza na akarukia vito kwa pupa. Lakini mara moja alisimama kwa mshangao.

Alijiona amekaliwa na uzito wa vitu alivyopapia. Juu ya uzito huo hakuweza kuongeza hata pini moja ya shaba.

Vitu vilivyobaki vilimtazama kama vilivyokuwa vikimsimanga choyo yake. Tamaa ya mali ni kubwa. Mioyo mingi haitoshwi na mali. Walakini, kwa kweli fikira ya mali isiyo kadiri ni mzigo usiochukulika.

Alipotoka pale aliingia katika maduka ya majohari. Huko aliona wenyewe wamekaa vitini. Mbele ya kila tajiri lilikuwako bweta. Mabweta hayo yalijaa yakuti, almasi, fususi, lulu, feruzi na mahohari mengine. Matajiri wote walikuwa mawe. Alitupa chini vito vilivyotengenezwa , akachagua yakuti; aliacha yakuti akashika almasi; alikataa almasi akatwaa fususi; alitaka lulu badala ya fususi, na feruzi kwa majohari mengine.

Alikuwa hana nguvu ya kuchukulia majohari yote. Kiasi cha majohari alioweza kuchukua hakikupunguza wingi alioukuta. Majonzi yalimjia,

akasikitika juu ya ndugu zake kwa kukosa kufuatana naye. Ndugu zake walikuwa na miguu ya kuendea bali hawakuitumia; walikuwa na nguvu za kuchukulia tunu za kutosha kwa utajiri wao lakini hawakuwapo.

Hili lilimuonesha Adili kuwa maumbile yalikuwa si bahili. Yalikuwa karimu katika kugawa vipawa. Lakini zaidi ya nusu ya hasara za mwanadamu hutokea kwa sababu wenyewe hwataki kutumia vipawa vyote walivyopewa. Basi alichukua alichoweza akendelea mbele. Moyo wake ulijaa majuto juu ya ndugu zake aliopenda kushirikiana nao furaha ya ugunduzi, fahari ya usitawi wa utukufu wa matendo bora.

Alipozunguka nyuma ya maduka alitokea kulikokuwa na nyumba moja kubwa kabisa. Nyumba yenyewe ilikuwa na milango mingi. Miongoni mwa milango hiyo mmoja ulikuwa ni mkubwa sana. Kwanza hakufahamu kwanini mwenyewe alipata gharama kubwa juu ya milango mingi kama ile. Kisha aliona kuwa gharama yake ilikuwa na maana kwa mtu mwenye akili. Si nyumba tu, hata katika jambo lolote hadhari hukataza mtu kujitia ndani yake kama halina milango ya kuingilia na kutokea. Milango ya nyumba ile ilitosha kwa usalama.

Baada ya kuwaza hivyo alipita kwa mlango mkubwa uliokuwa wazi, akaona mabawabu na askari waliokuwa na sura za kuogofya. Lakini walikuwa mawe.

Ndani kulikuwa na uwanja mkubwa uliozungukwa na viti pande zote.

Aliendelea mbele kidogo akatokea katika halmashauri kuu. Juu ya halmashauri hiyo palijengwa ulingo. Ulingo wenyewe ulikuwa umejengwa kwa ustadi mwingi. Juu yake palizunguka watu aliodhani kuwa mawaziri, makadhi, mashehe, wanajimu, washauri na madiwani wengine.

Kati yao palikuwa na kiti cha dhahabu kilichotonewa kwa majohari mbalimbali. Juu ya kiti hicho alikaa mfalme aliyevaa libadi za fua zilizokuwa hazitazamiki kwa kumetameta. Kichwani mwake alivaa taji. Taji hilo lilipangiliwa kwa majohari ali ali. Kwa mng’ao mkubwa wa majohari mfalme mwenyewe alikuwa hatazamiki. Alipopanda juu kutizama aliona hadhara yote ilikuwa mawe matupu.

Alishuka chini akaingia katika halmashauri nyengine.

Hiyo kadhalika ilikuwa sawasawa na ile ya mfalme ila ilikuwa na madiwani wa kike watupu. Baadhi ya madiwani walikuwa wamesimama mbele ya malkia na mikono yao vifuani, na wengine walikuwa wamepiga magoti chini yake kwa unyenyekevu. Walakini halmashuri hiyo ilikuwa bora kuliko ile ya kwanza.

Ilikuwa na meza za pembe na viti vya mpingo. Juu ya meza palikuwa na bilauri za johari memetevu. Halmashauri nzima ilikuwa imejaa wanawake waliokuwa na uzuri wa sifa kubwa sana. Malkia mwenyewe alikuwa amekaa kitako kati yao.

Mabibi wote walikuwa mawe matupu. Utulivi wa akili wa Adili ulichafuka. Alitupa chini majohari yote yaliyokuwa katika miliki yake. Moyo wake ulisimama juu ya bilauri zilizo mezani. Alichukua zilizotosha kuwa mzigo wake akaondoka pale kabla moyo haujarogwa na uzuri wa mabibi waliogeuka mawe.

## MRITHI WA MJI WA MAWE

Baada ya kwenda hatua chache Adili aliona mlango mdogo. Kizingitini pake palikuwa na ngazi iliyoongoza juu. Alipopanda vidato vichache aliona dalili za mtu au watu walioishi mle. Kwanza alikuwa anapanda kwa kusitasita, lakini sasa dalili zile zilimvuta akafululiza kupanda.

Aliendа mpaka orofani. Alifuata zilikoongoza dalili mpaka akafika kulikokuwa na chumba kidogo. Mlango wake ulikuwa wazi, kwa hivi aliingia ndani.

Huko aliona pazia la hariri lililotaraziwa kwa vito vya dhahabu, lulu na yakuti linaning'inia mbele yake. Fususi hizo zilimetameta kama nyota. Dalili alizoona ziliendelea nyuma ya pazia. Alijipa moyo mkuu akafunua pazia. Alipofanya hivyi macho yake yaliona mlango wa tarabe. Mlango huo ulikuwa mzuri sana. Mbao zake zilikuwa za mpingo, nazo zilinakshiwa kwa johari na pembe. Mtu yeyote angeliona mlango huo angestaajabu sana. Adili alibisha hodi akaingia katika chumba kikubwa. Chumba chenyewe kilikuwa kimepambwa vizuri sana. Katikati palikuwa na meza na kiti. Msichana wa fahari alikuwa amekaa kitako pale juu ya kiti. Uso wake ulikuwa umetukuka kwa uzuri uliokuwa haumithaliki.

Bila shaka yeye alikuwa malkia wa wazuri katika dunia nzima. Libasi alizovaa zilikuwa na thamani kubwa sana. Katika miji yote mingine aliyopata kufika katika safari zake, Adili alikuwa bado kukutana na mtu yeyote mwengine aliyevaa libasi nzuri kama zile.

Kama uzuri ulio peponi wamejaaliwa malaika, karibu uzuri wote duniani alijaaliwa msichana huyo. Uzuri wake ulikuwa haulingani na uzuri wa mwanamke yeyote aliyesifiwa kuwa mzuri katika zama zake. Msichana mwenyewe alikuwa anasoma kitabu kitakatifu. Matamko yake yalikuwa kama mafuatano ya muziki.

Moyo wa Adili ulitekwa na mapenzi ya tamasha hiyo.

Akili yake ilipotea na nuru ya macho yake ilizimika kitambo. Ile ilikuwa mara ya kwanza mshale wa mapenzi kupenya moyoni mwake. Ulipenya

katikati ya moyo wake.

Haukuwacha nafasi ya mapenzi ya mwanamke mwengine. Licha ya Adili, hata mtu mwengine aliyekuwa hajui mapenzi angalikutana na mwanamke huyo moyo wake ungalitekwa pia.

Akili ya Adili iliporudi alimwamkia mwenyeji wake. Mwenyeji aliyeamkiwa hakuitikia tu, alitaja jina la aliyemwamkia vilevile, akamkaribisha kwa furaha. Adili alimuuliza alilijuaje jina lake, yeye alikuwa nani na muujiza gani uliopita pale hata viumbe wa mji mzima wakageuka mawe. Bila ya kusema neno msichana aliondoka akaenda kuchukua kiti. Alikiweka karibu yake na kumuomba Adili akae kitako. Mwendo aliotumia katika kwenda na kurudi wakati wa kuchukua kiti ulichukua pumzi zote za Aduli. Alikwenda kwa hatua za kupendeza, na mikono yake ilipunga kama upepo.

Uzuri wake wa fahari ulikuwa na madaha makubwa. Chumba chake kilikuwa kama mahali pa faraja panapotafutwa na wanadamu.

*Miguu ya msichana na mwendo aliokwenda,*

*Adili alipoona,*
*moyowe ulimshinda.*

*Alikuwa na miguu mfano wa charahani*

*Watu wa ulimwengu huu*
*Hajatokea kifani.*

*Alipendeza hatua*

Wakati alipokwenda,

Chini viatu chalia

Mithali ya kinanda

Alikwenda kwa madaha

Mwanamke mwenye enzi,

Yaliyompa faraja

*Kila mwenye kubarizi*

# MJI ULIVYOGEUKA MAWE

Sasa msichana alieleza kwamba alikuwa binti mfalme, jina lake lilikuwa Mwelekevu. Baba yake, mfalme Tukufu, alikuwa yule aliyeonekana kitini katika halmashauri ya madiwani wanaume. Mama yake, malkia Enzi, alikuwa yule aliyeonekana katika halmashauri iliyohudhuriwa na madiwani wanawake. Ufalme wao ulikuwa na utukufu mwingi na nguvu nyingi.

Labda dola yao ilikuwa ya kwanza duniani iliyokuwa na miji laki saba. Isipokuwa, Fahari, mji uliogeuka mawe, miji mingine yote ilizama baharini. Raia chini ya bendera yao walikuwa lukuki. Mawaziri walikuwa laki tano. Kila waziri alikuwa na umati wa watu. Amiri jeshi mmoja alikuwa na majemedari elfu moja na sufufu ya majeshi. Hazina za nchi zilikuwa na mali zisizohesabika kama machimbo ya Tanganyika.

Ulimwengu uliajabia dola yao, ushujaa wa askari na busara ya mawaziri wao. Walakini, juu ya sifa hizo, mfalme, malkia na raia walikuwa waabudu mizimu. Mizimu yao ilikuwa miti. Miti yenyewe ni ile iliyogeuka mawe ukutani. Kabwere, mganga na imamu wa mizimu hiyo alivuta mioyo ya watu wote. Siku moja asubuhi mfalme na malkia walikwenda katika halmashauri zao, kila mmoja akakaa juu ya kiti chake.

Madiwani walikuwa wamewazunguka kabla ya kuanza kazi zao za desturi; mtu mmoja ambaye hakukulikana alipotoka alisimama ghafula mbele ya mfalme, akajitangaza kuwa aliitwa mrefu.

Mrefu alikuwa muujiza katika viumbe. Alikuwa na miguu mikubwa na mapaja manene, kiuno cha utambo na kifua kipana; shingo yake ndefu ilichukuwa kichwa kikubwa.

Mabega yake ya mraba yalining’iniza chini mikono iliyokuwa na nguvu kama manjanika. Kwa kimo cha kukithiri, alitembea bila kuguswa na maji magotini, akafikia vilele vya milima kwa mikono yake. Aliweza kukamata ndovu chini au nyangumi baharini akamuoka kwa jua mbinguni. Sauti yake ilikuwa kama radi. Kwa wepesi wa ajabu wa kuzunguka dunia kwa sekunde moja, alionekana kama kiumbe kilichoumbwa maalum kuokoa kitu motoni, baharini au katika hatari nyengine.

Mrefu alimwambia Tukufu kuwa mfalme ni naibu wa Mungu duniani. Kwa hiyo, ufalme ni amana kubwa. Amana hiyo ilitaka uangalifu mkubwa kwa sababu ni dhima bora iliyowekwa mikononi mwa wanadamu. Wajibu wa kwanza wa mfalme ni kuwa muadilifu katika matendo yake.

Kila tendo, jema au baya, ni mfano kwa raia wake. Kwa sababu ya maisha ya milele, ibada ya mizimu ilikuwa maangamizi, na uimamu wa ukabwere ujinga mtupu.

Tukufu alimtazama msemaji kisha akasema kwa ukali, "nini kilichokujulisha kusema upuuzi, Mrefu"? Kama kwa sababu ya urefu ubongo wako umeyeyuka kwa jua, kaa kitako chini ya kivuli cha mizimu yetu utaburudika. Kama umerogwa, Kabwere atawakomesha waliokuroga. Riziki ya wanadamu hutoka mimeani. Kwa sababu hiyo, mimi na kaumu hii twaabudu miti. Funga ulimi wako bwana. Usipofunga hasira ya mizimu itakuwa juu yako."

"Tafadhali jiokoe" mrefu alionya. "Hapana haja ya jibu la haraka. Tumia wakati upendao kufikiri. Nimesema neno la Mungu. Mungu hachelei tisho la mwanadamu, kazi ya mikono yake mwenyewe. Neno takatifu ni gumu kufahamika, lakini lina tija kwa wajisumbuao kulifasiri. Kila msaada nitakupa wa kulifasiri"

Tukufu hakujali onyo hili, akaamrisha kushikwa kwa mrefu aliyekuwa hasogeleki wala hashikiki. Uwezo usio hadhari ni kileo kibaya sana. Siku ile ilikuwa ya tisho na msiba, ole na maangamizi makubwa. Kwa laana iliyotamkwa na mrefu, miji mingine yote ya dola hii iligharika na kila kiumbe kilichokuwa na maisha katika fahari kiligeuka jiwe.

Hili lilipotokea Mwerevu alikuwa darini anachungulia nje kupitia dirishani. Toka pale aliweza kumuona mrefu na kusikia maneno yake. Hakupendelea kushindwa kwa baba yake. Hapana mtoto apendaye hili. Walakini, mapendeleo yakiachwa mbali, nuru ya fikira humulika mno siku zote juu ya kweli kuliko uongo, na juu ya haki kuliko dhuluma. Nuru hii ndiyo iliyomwokoa Mwerevu katika maangamizi yale ya kutisha.

Na tangu siku ile aliamini kuwa onyo la bure likikataliwa huleta majuto ya milele.

Haya yalipokwisha jiri, Mrefu alimpa binti mfalme chuo kitakatifu alichokisifia kuwa bora kuliko vitabu vyote vya duniani vikichanganywa pamoja. Kwa matumizi mengine, Mrefu aliomba mkomamanga uote,

Mkomamanga huo ulizaa komamanga moja kila siku. Kila chembe katika komamanga hilo lilikuwa chakula na kinywaji mbalimbali.

Kwa mti ule wa ajabu, binti mfalme aliweza kuishi maisha ya faraja. Mwisho alionywa kuwa siku ya kuona mti ule umezaa matunda mawili ajue Adili, mwokozi wake amefika. Hilo ndilo lililomjulisha siku ile mgeni wake alikuwa si mtu mwengine ila Adili.

Usemi wa binti mfalme ulimuonesha Adili kuwa turufu huenda kwa mchezaji siku zote. Laiti asingalikwenda wenziwe walikoogopa akatafutatafuta, asingalikutana na bahati ambayo hakutazamia kuja katika ndoto zake. Alimchukuwa binti mfalme pamoja na tunu bora alizoweza. Katika tunu yake pia yalikuwepo makomamanga mawili ya ajabu. Hayo yalikomesha kiu na njaa katika merikebu yao kwa muda wa siku kadha wa kadha.

Adili aliyageukia manyani akawauliza yaliyosemwa yalitokea au hayakutokea. Manyani yalificha nyuso zao kwa viganja vya mikono yao kwa aibu.

KUTOSWA KWA ADILI

Nadhira na mabaharia walimshangilia Adili kama mtu wa bahati ya peke yake, na kuwa mtu mwengine yeyote kati yao angalifuatana naye waliogopa asingelikutana na bahati ile kubwa. Adili aliwashukuru wote akisema kwa furaha, “mkulima alikuwa mmoja siku zote, lakini walaji wengi” pato lake lilikuwa pato lao vilevile.

Aligawa tunu zake katika mafungu manne yaliyokuwa sawasawa. Fungu la kwanza alimpa nahodha, na kila ndugu yake akapata fungu moja. Fungu lililobaki lilikuwa lake mwenyewe. Hili aliligawa tena katika mafungu mengi, kila baharia akpata sehemu yake.

Isipokuwa ndugu zake, watu wote chomboni walimwombea heri. Nyuso za ndugu zake zilionekana kukunjamana na macho yao yaliiva. Alifahamu hawakuridhika kwa choyo chao kikubwa.

Aliwataka radhi akawaambia kuwa ingawa mafungu yao yalikuwa madogo, lakini wao walikuwa ndugu zake, mali yake ilikuwa yao katika maisha na mauti. Palikuwa hapana sababu ya kukasirika.

Wakati alipokuwa akiseam hayo na ndugu zake stahani, Mwelekevu alikuwa amekaa ngamani na jahazi ilikuwa ikienda moto mmoja.

Sasa Hasidi na Mwivu walimuuliza Adili nia aliyokuwa nayo juu ya bibi yule mzuri aliyempata katika mji wa mawe. Aliwajibu kwamba wakifika salama Janibu nia yake ilikuwa kumwoa. Hasidi aliomba kuwa angefurahi kama angemwoa yeye bibi yule.

Mwivu pia alinasihi kuwa angalipenda kumwoa yeye.

Kwa kusikitika, lakini kwa imara kabisa, Adili alijibu kuwa kama walitaka neno jingine lolote katika miliki yake angaliwapa, ila hakufikiri kuacha mkono wa bibi yule kuguswa na mtu mwengine katika ndoa ila yeye mwenyewe. Wao walimtaka lakini yeye alimpenda zaidi. Walakini wakirudi Janibu atawatafutia mabibi wawili wazuri. Gharama yote itakuwa juu yake. Harusi zao na yake zitakuwa siku moja.

Ndugu zake walihoji kama mume mmoja katika Afrika aliweza kuoa wake wengi, na mke mmoja katika Asia alipata kuolewa na wanume kadhaa, isingekuwa vyema kama ndugu watatu wa Janibu wangeshiriki uzuri wa mke mmoja?

Adili alibisha kwamba kuna mambo yanayofaa na yaliyokuwa hayafai kushiriki. Ndoa ilikuwa jambo moja katika yale yanayokataa ushirika. Ushirika katika ndoa ulipasa wanyama na ndege. Mtu alitunzwa mno kuliko mnyama. Huchukiza akiishi katika maisha duni. Ilipasa watu wa wakati ujao katika Afrika Asia na Janibu kuishi katika maisha bora ya utu, na kuifanya dunia mahala pa kiasi, siyo ulafi na uchafu. Mwanaume hakukusudiwa kuwa fahali wa kila mtamba, wala mwanamke kuwa tembe, la kila jogoo.

Ushirika wa ndoa ulipofanikisha na uvundo wa kuchukiza duniani, ndugu zake walinyamaza kimya kama warioridhika, lakini moto ulikuwa ukiwaka mioyoni mwao. Usiku Adili alipokuwa amelala na jahazi linaenda mbio kwa pepo za omo, ndugu zake walikuwa macho.

Mawazo mabaya hurusha usingizi. Kuzinduka kwake usingizini Adili alijikuta amechukuliwa hangahanga, kufumbua macho aliona ndugu zake wamemfunga kifati. Mmoja alimshika kichwani na mwingine miguuni. Koo yake ilisongwa sana.

Aliwauliza kwa pumzi nyembamba aliyoweza kuvuta neno walilotaka kumtendea.

Alijibiwa “Huss, fedhuli wewe! Wauliza neno ulijualo. Koma saa! Tumesalitika na mapenzi ya mwanamke aliyeko chomboni. Tumekushauri kumwoa shirika. Umekataa. Huna budi kufa”

Alitoswa baharini kam kitu kilichokuwa hakifai.

Adili aliwageukia manyani akawauliza kama yaliyosemwa yalitokea au hayakutokea. Manyani waliziba nyuso kwa viganja vya mikono yao kwa aibu.

MWOKOVU WA ADILI

Adili alipotupwa baharini alizama kama jiwe katika kina kirefu cha bahari ambacho urefu wake haukutambulika. Viwambo vya masikio yake vililia akadhani maji yalipenya sikio hata sikio, na mianzi ya pua yake ilijaa maji yaliyozuia pumzi. Macho yake yalipofumbuka vimetameta kama nyota mbinguni vilionekana katika maji. Vimetameta hivyo vilifanywa na mtikisiko wa mwili wake. Kutumbukia baharini usiku wa kiza ni hatari ya kutisha sana.

Kasi ya kutupwa ilipokoma alijitatamua akakata vifungo vya kamba aliyotatizwa mwilini mwake. Sasa mikono yake na miguu yake ilianza kufanya kazi. Nusu ya nguvu yake ilikuwa imetumika. Lakini matumaini yake yalikuwa kamili. Adili alikuwa si mkata tamaa, na kabla pumzi yake haijakwisha alikusudia kuibuka. Jaribu lake lilikutana na fanaka, maana kabla moyo wake haujakoma alijiona anaelea juu baharini.

Aliinua kichwa juu ya maji akahema kwa nguvu kama garimoshi.

Kulipopambazuka alikuwa katika bahari iliyogadhabika kwa dhoruba kali, na hali yake ilikuwa taabani. Kutazama hatari usoni kunavunja moyo wa mtu lakini alijikaza kiume.

Mara ile alikuja ndege aliyekuwa na umbile la kutisha akamuopoa Adili majini. Kama koleo miguu ya ndege ilimshika kwapani akaruka naye. Fikiri wewe mwenyewe hofu aliyokuwa nayo Adili. Binafsi yake alijiona ameokoka kuliwa na papa akawa chakula cha tai. Ndege mwenyewe alipaa juu mpaka Adili akapotelewa na fahamu. Fahamu yake ilipomrudia alijikuta katika nyumba kubwa sana iliyokuwa nzuri zaidi ajabu.

Wasichana warembo na waliochangamka walikuwa watumishi katika nyumba hiyo. Miongoni mwao palikuwa na bibi mmoja aliyejipambanua kama malkia. Huyu alikaa juu ya kiti cha enzi kilichopambwa na majohari mbalimbali. Rangi ya mavazi yake ilikua fua, na kichwani alivaa taji lililopigisha moyo mshindo kwa uzuri. Yule ndege alikuapo, lakini mara ile alijigeuza msichana wa mtanashati mkubwa. Msichana mwenyewe alikuwa yule aliyezama ardhini baada ya kuokolewa na Adili alipokuwa katika umbile la tandu na kushambuliwa na nyoka jabalini.

Malkia alimuuliza msichana mtu aliyemwokoa baharini alikuwa nani, na kwanini aliletwa mbele yake?.

Msichana alieleza kuwa mtu yule alikuwa mfadhili wake mkubwa. Zamani maisha yake yalipokuwa katika hatari ya nyoka alipata wokovu kwake. Alimuokoa na kumleta mbele yake kwa sababu aliahidi kulipa fadhili yake. Kusikia vile, malkia akasimama akampa mkono Adili aliyeupokea huku amepiga magoti chini. Malkia alimwinua akamkaribisha kitini akisema "starehe, mwanangu

Hali yako ni hali yetu".

Kisha msichana alimuuliza Adili kama aliweza kumtambua yeye alikuwa nani. Adili alijibu kuwa hakuweza. Msichana alieleza kuwa yeye alikuwa tandu katika jabali fulani zamani akakaribia kuuwawa na nyoka, lakini aliokolewa.

Adili alikubali kuwa alikumbuka kuwa aliona tandu jeupe, nyoka mweusi, na msichana aliyezama ardhini.

Tandu lilikuwa yule msichana. Naye alikuwa Huria binti Kisasi. Kisasi alikuwa mfalme wa majini. Aliyekaa kitini alikuwa mama yake. Jina lake lilikuwa Mjeledi malkia wa majini. Nyoka aliyepigana naye Huria alikuwa waziri wa ngazi, alijulikana kwa jina la Hunde.

Hunde alikuwa kiumbe cha mwisho katika wanaume waliokuwa na sura mbaya.

Siku moja katika matembezi Huria alikutana na Hunde. Alikuwa hatazamiki kwa ubaya, licha ya yeye kumtazama mtu. Pale pale Hunde aliingiwa na shauku kubwa juu ya Huria. Wanawake hukutana na mikasa mingi mibaya duniani. Mioyo yao hulemewa na haja zisizokubalika; masikio yao hutiwa uziwi kwa maombi ya haraka; miili yao ni mawindo ya jeuri daima

Hunde alikwenda kwa kisasi kumposa Huria. Kisasi alijibu kuwa Hunde alikuwa ni sufu kwa binti yake japokuwa alikuwa waziri wa ngazi, na kwamba asingalithubutu mbele yake haja kama ile. Tangu siku ile alikomeshwa tamaa ya kuposa mabinti wafalme. Aliudhika, akatisha

kumuonyesha Huria uwezo wake. Na tangu alipotisha hivyo hakumpa nafasi tena hata ya uzi kupenya tundu la sindano.

Kila mahali alipopita, hunde alifuata nyayo zake mpaka aligundua alikokuwa. Iliendelea hivyo mpaka Kisasi akapigana naye. Alishindwa akakimbia. Huria alipotaka kutembea alijigeuza umbo la mnyama. Kila alipojigeuza na yeye alijigeuza vilevile, akanusa harufu yake kama mbwa. Alipojigeuza panya, yeye alijigeuza paka, alipojifanya paka, yeye alijifanya chui, alipokuwa chui yeye alikuwa simba.

Kila alipoingila yeye alipajua kwa kufuata nyayo zake. Wanaume wana inda mbaya ufisadi unapowapofusha.

Siku aliyojigeuza tandu yeye, alikuwa nyoka akamfukuza. Alipochoka kukimbia alimkamata. Kabla hajamhasiri, Adili alimpiga jiwe akafa. Alijigeuza mtu akaonekana na Adili kwa macho yake. Kabla ya kujizamisha chini aliahidi kulipa wema kwa Adili.

Huria aliomba dua siku zote ya kuweza kutimiza ahadi yake kwa Adili. Siku aliyotoswa baharini na ndugu zake alikuja upesi kumwokoa katika hatari. Ilipaswa wazazi wake, mfalme na malkia wa majini kumkirimu mfadhili wake.

Alimwambia mama yake kuwa deni alilowiwa na Adili lilikuwa kubwa sana. Hakudai lilipwe lote lakini lipunguzwe kama lilivyowezekana.

Mjeledi alimwambia Adili kuwa wema wake haukuoza. Kwa kumuokoa Huria aliwatendea wazazi wake fadhila na heshima kubwa nchi ya majini. Ilikuwa zamu yao kumkirimu walivyoweza sasa.

Adili aliyenyamaza kwa muda mrefu alijibu,

“Deni langu limekwisha lipwa lote. Niliokoa maisha ya binti yako, nae ameokoa yangu. Hapana deni tena kati yetu”

Malkia wa majini alitabasamu akasema, ” usiseme kikembe mwanangu. Wema wako ulikuwa asilia, nawe ulitangulia kuutenda; wa binti yangu

ulikuwa wa kuigiza, naye ameutenda nyuma. Asili na uigaji ni vitu mbali. Havilingani wala havitalingana milele”

Adili alipelekwa katika hazina ya majini iliyokusanya utajiri wote wa ulimwengu. Johari ndogo katika hazina hiyo ilikuwa na uzito usiochukulika na Adili. Alipochaguzaa kuchukua alichokipenda hakuweza kuchagua chochote.

Malkia alisikitika akasema , “haidhuru!” Alishika simu akasema, ” naweza kusema na mfalme wa majini?”

Jibu lilikuja “naam, kisasi huyu! Nani mwenzangu?”

“Mjeledi, malkia wa majini ndiye asemaye. Adili amechaguzwa apendacho katika hazina yetu, lakini ameshindwa kuchukua kitu cha uzito wa sindano moja. Wanadamu hawajaweza kutumia uwezo waliopewa kama majini. Nataka msaada wako”

“Vema, mlete hapa”. Kengele iliashiria. Adili alikwenda katika halmashauri ya majini. Alipofika mfalme alikuwa amekaa kitini kwa juu kuelekea hadhara kubwa ya mawaziri. Joho la mfalme lilikuwa la rangi ya fua, na kichwani alivaa taji la zari. Mawaziri walivaa majoho meusi, na vichwa vyao vilikuwa wazi.

Hadhara nzima ilisimama Adili alipotokeza. Alipokaa kitako alipewa kitabu cha hawala ya hazina ya majini. Kwa kila hawala iliyoandikwa na kutiwa shihi ilipochomwa Adili aliweza kupata alichotaka katika hazina ya majini. Alifurahi kwa zawadi ile. Ilikuwa nyepesi kuwekeka, rahisi kutumika, nayo si nzito kuchukulika. Alimshukuru mfalme wa majini akarudi kwa Huria.

Aliyageukia manyani akayauliza kama yaliyosemwa yalitokea au hayakutokea. Manyani yaliziba nyuso zao kwa viganja vya mikono yao kwa aibu.

NDUGUZE KUWA MANYANI

Baada ya Adili kutoswa nahodha akashituka, akauliza nini kilichotumbukia baharini kwa kishindo kikubwa. Kusikia vile ndugu zake wakaanza kujiliza uongo kuwa ndugu yao amepotea. Nahodha alikwenda kutazama akaona Adili hayupo. Aliamuru kutua nanga na kuteremsha mashua.

Lakini sasa dhoruba kali ilianza, na chombo kilikuws katika mrama mkubwa, kwa mawimbi makubwa na umande, kilipakia maji, omo na tezi, na kulia na kushoto.

Giza kuu lilinyemelea roho za mabaharia. Palikuwa. Hapatiliki nanga. Kwa hivi tamaa ya kumuokoa Adili ilikatika.

Nahodha alipotaka kujua Adili alivyopotea, ndugu zake walimwambia kuwa ndugu yao aliamka na kwenda msalani. Ghafula walisikia anguko kubwa majini.

Watu wote jahazini walisikitika kupotelewa na Adili. Ndugu zake walilizana kitambo wakanyamaza. Kilio cha kujisingizia hakina machozi wala matanga.

Hasidi na Mwivu walichukua sanduku la Adili na kulifungua. Walitoa majohari yote na wakagawana mafungu mawili na kuyagawa usiku uleule. Sasa ugomvi wao ulianza juu ya yule msichana mzuri aliyekuwa chomboni. Hasidi alitaka kumwoa, na Mwivu kadhalika alitaka kumwoa. Asiyefurahia heri ya mwenziwe, shari yake kumhadhibikia. Walimsahau ndugu yao aliyepotea dakika chache zilizopita kama aliyekufa miaka kumi iliyopita. Walikuwa na mioyo migumu iliyoje!.

Mwelekevu, yule msichana mzuri, alikuwa hana tabasamu. Uzuri wake ulisawazika kwa machozi ya njia mbili usoni. Huzuni ilimshika vibaya, lakini alikuwa imara kutetea heshima yake. Aliwaambia wale ndugu wawili wasigombane bure.

Hakuwa tayari kuolewa na yeyote kati yao. Na kabla ya sauti ya maneno aliyosema haijaishilia masikioni mwao, alijitosa baharini akatoweka vilevile.

Hasidi na Mwivu hawakujua la kutenda. Atakae makaa ya mgomba hapati kitu ila jivu tupu. Ndugu hawa wawili walimtosa ndugu yao kwa tamaa ya kumpata msichana, lakini walipata aibu tupu. Walikaa kitako wakifedheheka. Walikuwa katika hali hiyo na jahazi inakwenda mbio, Huria na Adili walitua ghafula chomboni.

Marejeo ya Adili yaliwashangaza watu chomboni. Macho ya ndugu zake yalisutana. Kwa kutahamaki walimkumbatia wakijifanya kumfariji. Walisema hatari yake ilitisha, na msiba wao ulikuwa mkubwa. Watu wengine wote chomboni waligeuza macho yao kando waliposikia uongo wa ndugu zake. Walakini Adili aliwashukuru akisema bahari haiweki amana ya kitu kieleacho. Kwa kuwa alielea aliokoka.

Kwa hasira kubwa Huria alinena, “kama mngalijua hatari ya kumtosa mtu baharini, au mngalikuwa na fikira za msiba, msingali jaribu kumtumbukiza ndugu yenu baharini alipolala.

Wauaji ninyi hamstahili kuishi”. Aliwashika shingoni pamoja na mkono wa kushoto, akawabana kwa nguvu za ajabu. Mkono wake wa kulia uliinua ngumi juu tayari kuwaangukia kwa uzito mwingi. Ndimi vinywani na mboni machoni mwao zilitoka kwa hofu wakataka kuombewa.

Damu nzito kuliko maji. Hadidi na Mwivu walikuwa damu kwa Adili, hakuvumilia kuona hilaki yao, akamuomba Huria kuwasamehe. Walimtosa tu, hawakumuua. Huria alibisha kuwa walistahili kifo. Jaribu la jinai lilitosha kuhalalisha adhabu ya kifo ujinini.

Adili alitaradhia kuwa jaribu la jinai halikutosha kuhalali kifo duniani. Kama walikufa kwa sababu yake angalikuwa mnyama wa mwitu mbele ya macho ya watu. Huria aliposikia hayo alinena sheria ya wanadamu ilitatiza. Kwa sababu hiyo walikuwa hatarini milele. Walakini alikubali kuwasamehe kwa sharti la kuwageuza wanyama. Aliwalaani watoke katika umbo la uanadamu. Mara ile ndugu zake walikuwa manyani.

Kisha Huria aliwakabili watu waliokuwa chomboni akasema Adili alikuwa rafiki yake mkubwa.

Alimjali na kumuheshimu juu ya marafiki zake wote. Alipata upendo wake kwa sababu alikuwa sahili na mstahiki wa kuajabiwa na dunia nzima. Ataonana naye mara kwa mara. Mtu yeyote akifitini ataona nguvu ya mkono na uwezo wa ulimi wake.

Atampatiliza kama alivyofanya kwa waovu wale wawili. Wajihadhari wapate kujiokoa kwa sababu alikusudia kutimiza aliyosema. Aliwaonya kuwa watakapofika kwao wasiseme habari ile Mtu yeyote atakayejaribu kunong'ona habari ile atakoma kusema milele.

Aliagana na Adili akasema, "funga manyani haya kwa kamba. Ukifika Janibu utayafunga kwa minyororo viunoni mbalimbali. Utayatia chumbani na kila moja lifunge peke yake. Kila usiku wa manane utachukua kiboko ukafungue kila nyani ulipige mpaka lizimie.

Utayapa posho na kuyaadhibu hivyo daima. Kama amri hii haikutiiwa, utaadhibiwa wewe".

Alipokuwa akitoa amri hii alikuwa anajibadilisha sura za ajabu kila dakika moja. Watu wote jahazini walishikwa na mshangao mkubwa kwa mabadiliko yale ya mfululizo.

Wakatosheka kuwa liliweza kubadilisha kitu chochote katika umbo lililotaka.

Adili aliyageukia manyani akauliza kama yaliyosemwa yalitokea au hayakutokea. Manyani yaliziba nyuso kwa viganja vya mikono yao kwa aibu.

## ADHABU YA KWANZA

Baada ya kutoweka kwa Huria. Adili alikwenda ngamani kumtazama Mwelekevu. Hakuona mtu. Alipouliza aliambiwa alijitosa baharini ndugu zake walipomkalifu kumuoa. Adili hakuweza kujizuia, akaanguka chini kwa huzuni. Moyo wake ulifumwa kwa msiba akalia kama mtoto mdogo.

Uzuri aliotetea kwa dhamana ya maisha yake ulipotea. Aliona wokovu wake haukumfaidia. Bahati ilikuwa mbaya na katili sana kwake. Alifikiri kwamba yeye peke yake ndiye aliyepatwa na ajali mbaya kama ile tangu kuumbwa kwa dunia. Adili aliwaza hivyo, haujulikani mtu mwengine angewazaje.

Kulipokucha chombo chao kilitia nanga Janibu.

Matajiri walipanda chomboni wakaamkiana na Adili. Walizungumza mambo mengi, lakini hapakuwa na mtu hata mmoja alieuliza habari za ndugu zake. Hili lilimshangaza, akamaizi kuwa watu walio aili walikuwa hawana nafasi katika kumbukumbu za dunia.

Alishuka pamoja na manyani yake akaenda zake nyumbani kwake. Baada ya kuyaweka chumbani alijishughulisha na kupakuwa mali yake. Hakuwahi kutafuta minyororo ya manyani siku ile, na usiku alisahau kuyapiga akalala. Saa saba usiku Huria alitokea na hasira imemjaa tele. Alisema kuwa alikuwa jini, neno la jini halirudi. Kwa kukosa kutii amri yake adhabu ya kwanza ilimpasa Adili.

Kabla Adili hajajibu neno, mikono yake miwili ilikuwa katika mkono wa kushoto wa Huria. Hakuweza kuponyoka. Kwa mkono wa kulia Huria alimpiga Adili kibao mpaka akazimia. Ndipo alipokwenda yalipokuwa manyani akayapiga kiboko vilevile yakakaribia kufa. Alimrudia Adili aliyekuwa anaanza kupata fahamu akasema.

“Twaa kiboko hiki, utayapiga manyani haya kesho usiku kama nilivyofanya. Siku moja ikipita bila kuyapiga, kiboko hiki kitaishia mwilini mwako”. Macheche ya moto yalitoka kinywani mwake alipokuwa akiamuru hili, na mara neno la mwisho lilipotamkwa alitoweka.

Siku iliyofuata Adili alikwenda kwa sonara akatengeneza minyororo miwili ya dhahabu. Aliileta nyumbani kwake akaifunga viunoni mwa manyani yake. Usiku alipokwenda kuyapiga na kuyaposha, machozi yalimlengalenga machoni. Katika ini alifumwa na mishale, na moyoni mwake mishomo ya maumivu makali. Hakupendelea kuadhibu wanyama waliokuwa kwanza ndugu zake. Huruma yake ilikuwa kubwa lakini alikalifiwa na amri.

Huria alijua huruma ya Adili na kuwa alimkalifu sana. Lakini ndugu zake walikuwa waovu, katili, hiani na wauaji wa kutisha. Walikosa fikira wakawa duni kama wanyama wa porini. Adhabu kali kwa waovu ilikuwa ndiyo ulinzi peke yake ya wema. Jini aliliona hivyo, haijulikani mtu angelionaje.

Siku nyingi zilizopita Adili alidhani labda adhabu ya Huria ilikwisha.

Siku moja hakuyapiga manyani yake. Lo salale! Zahama gani? Alijuta kuzaliwa, akatamani ardhi ipasuke ajitie ndani yake. Alipigwa kiboko siku hiyo kuliko siku ya kwanza. Mwili wote ulienea makato ya kiboko, ukavuja damu mpaka akazirai.

Aliteremsha mavazi aliyovaa mpaka kiunoni akaonesha makovu ya mapigo ya Huria. Wepesi wa maumbile wa kuondoa alama haukuweza kufuta makovu ya Adili. Yalijionyesha waziwazi mwilini mwake. Toka siku ile na baadaye hakusahau maumivu ya mapigo yale. Kwa muda wa miaka kumi hapakupita tena hata siku moja aliyoacha kuyapiga manyani yake. Kwa huruma yake kila mara baada ya kuyapiga, aliyanasihi akilia

*Nala sumu ndugu zangu,*
*msambe naona tamu*
*Takalifu kubwa kwangu,*
*kuadhibu yangu damu*
*Sina raha ndugu zangu*
*Neno hili kwangu gumu.*

Mwisho wa ushahidi, Adili aliyageukia manyani akauliza kama yaliyosemwa yalitokea au hayakutokea. Manyani yalijiziba nyuso zao kwa viganja vya mikono yao kwa aibu.

## KULA NA MANYANI

Wafalme hukutana na mambo magumu kabisa katika maisha yao. Wako walioanza maisha katika unyonge na dharau, wakapanda mpaka juu ya kilele cha heshima na utukufu, waliozuka katika usahaulifu wakajitia katika makumbusho ya milele, waliotoka katika maisha ya tufani wakaenda katika maisha ya shwari, walioshinda vita vikuu, walioongoza watu katika maendeleo bora na nchi katika upeo wa wasitawi.

Lakini wako wafalme wachache sana waliopata kukutana, kama Rai, na dawaa kati ya watu na majini, jambo hili lilikuwa moja ya majaribu magumu kabisa.

Rai alijua manyani yalikuwa wanyama waliofugika na kufundishika. Kwa hivi, alituhumu isije kuwa manyani yale yalifugwa na kufunzwa kuziba nyuso wakati bwana wao aliposema. Adili alikuwa mwanadamu; na mwanadamu haishiwi na uchafu kama kilihafu.

Hapana mtu mwema aliyetayari kuungama kosa makusudi ili aadhibiwe. Adili alikuwa mbele ya sheria juu ukatili kwa wanyama. Aliweza kusema na kujitetea, lakini manyani yake yalikuwa hayawezi. Maneno yake yalipasa kuchunguzwa kwa ushahidi wa Huria.

Kupatikana kwa ushahidi ule kuliwazika, lakini hakukutazamiwa kuwezekana. Huria alikuwa jini; si mwanadamu. Jini kutii mwanadamu lilikuwa jambo geni, lakini alijifunga kulijaribu.

Alifikiri kama dhuluma aliyotendewa Adili ilikuwa kubwa, na adhabu waliyopata ndugu zake ilikuwa kubwa pia. Kama Adili alikaribia kuuawa, na ndugu zake walikuwa katika dhila ya unyama. Pande zote mbili ziliteswa na majaribu makubwa.

Sasa ilikuwa zamu ya kujaribiwa mamlaka ya ughaibu kama pande mbili zilivyojaribiwa.

Kwa hivi, Adili aliulizwa kama aliweza kuwasamehe ndugu zake. Neno hili lilikuwa gumu kukubalika, lakini Adili alilikubali mara lilipotoka kinywani

mwa mfalme. Adili alikuwa si mtu wa ovyo. Moyo wake ulihitilafiana sana na mioyo ya watu wengine.

Alikuwa na moyo mwema usiokata tamaa, mvumilivu, mwenye huruma, uliotayari kusamehe. Kama nusu ya watu duniani wangekuwa na mioyo kama wa Adili, nusu ya mashaka yao ingetoweka na bila shaka wangeishi maisha ya peponi hapa katika ardhi.

Sasa Rai alichukua daraka la kuokoa yale manyani mawaili katika unyama. Yakiokoka na kuwa watu tena atawapatanisha na ndugu yao waishi maisha mapya pamoja kwa amani. Alitoa amri kuwa Adili arudi Janibu na manyani yake, kwa sharti kuwa usiku ufuatao hatayapiga. Walakini Adili alichelea kama hatayapiga usiku ule mapigo ya Huria yatamwangukia yeye mwenyewe.

Aliona mwili wake haukuweza kuhimili hata mguso mdogo. Itakuwaje kama itamlazimu kupigwa! Rai alipojulishwa hili alimshauri Adili kujasiri. Bila ujasiri nadra mtu kufanikiwa.

Kama hakusamehewa kupigwa, ilimpasa kuvumilia adhabu ya usiku mmoja. Aliandika barua akampa Adili ampelekee Huria. Barua yenyewe ilikuwa fupi lakini ilisadifu madhumuni, ikasema hivi:

Falalati Huria,

*Binti mfalme wa majini*

Daawa ya Adili na ndugu zake waliogeuzwa manyani ipo mbele yangu inangoja hukumu. Adili amekubali kupatana na ndugu zake. Walakini mapatani yao hayakamiliki mpaka wewe umewaopoa katika dhima ya unyama. Kama msaada wako utapatikana juu ya shauri hili. Ughaibu itakuwa tayari kusaidi mashauri ya ujinini. Kwa kusaidiana hivi, suluhu inayotafutwa sana kati ya wanadamu na majini itapatikana. Suluhu ya wafalme wa viumbe ni kiungo cha mapatano ya raia. Kila mfalme, malkia na raia huhitaji suluhu hii. Itakuwa fahari kubwa iliyoje kama mimi na wewe tukilianzisha jambo hili! Tafadhali ondoa laana uliyotamka kwa ndugu zake Adili. Kama kesho nikiwaona wamekuwa watu tena nitakushukuru sana.

Fulali Rai

*Mfalme wa Ughaibuni*

Adili aliporudi Janibu aliyachukuwa manyani akayatia katika chumba kimoja katika nyumba yake wenyewe naye akaenda katika chumba kingine. Huko aliwaza kuwezekana kwa mapatano ya Rai na huria. Kama hawatapatana ghadhabu ya Huria Haivumiliki.

Alikaribia kukata tamaa, lakini alitahayari mwenyewe alipojiona kwamba amekuwa maskini wa saburi. Mwenye saburi hukidhiwa haja zake. Mbona yeye alikuwa hana? Alitingisha kichwa chake kama aliyekuwa akikataza wazo la kukata tamaa. Hasidi na Mwivu walikuwa ndugu zake mwenyewe. Sadaka ya kwanza katika jitihada ya kuwaokoa ililazimu kutoka kwake yeye, sio kwa mfalme wala jini. Katika fikira hii alijiandaa asiyapige manyani usiku ule kama Huria atakuja kumpiga yeye mwenyewe itakuwa kama kwamba amewapumzisha ndugu zake kwa adhabu ya usiku mmoja.

Aliendelea kufikiria kuwa Rai alikuwa ametukuzwa kwa ufalme wa hekima. Asingaliweza kumshauri kujitia katika hatari kubwa namna ile kama kulikuwa hapana njia salama.

Sasa katika masikio yake alisikia kama kwamba sauti ikimnong'oneza kuzidi kusubiri na kujiweka tayari.

Tazama adhama na tabia ya Adili. Alikuwa tayari kujikalifu takalifu ilipolazimu, kujidhabihu dhabihu ilipotakiwa; na kusamehe msamaha ulipobidi. Akili yake ilipenya katika mambo, ikazunguka na maisha. Alikuwa muungwana kila kiungo cha mwili wake. Matendo makubwa na bora kuliko yaliyotendwa zamani yangetendwa sasa kama kila mtu angefikiri kama alivyofikiri Adili.

Alikwenda katika chumba kilichokuwa na manyani, akayafungua minyororo viunoni mwao. Alisema nayo polepole kuwa majonzi yao yanakaribia kwisha, yeye mwenyewe aliwasamehe; mfalme Rai alikuwa akijaribu kuwaokoa katika balaa iliyowapata. Usiku wa siku ile taabu yao itakoma. Manyani yalichangamka, yakarukaruka kwa furaha yakimshikashika Adili miguuni. Kwa kuyaona manyani katika hali ile , Adili aliyapapasa akacheza nayo mpaka wakti wa chakula cha usiku.

Chakula kilipokwisha wekwa mezani pamoja na ala za kulia, watumishi walisimama kumngojea.

Aliyaambia manyani kukaa vitini. Yaliruka juu ya viti yakakaa kitako. Mikia yao ilikuwa ikining'inia chini. Adili alipochukua kijiko, uma au kisu kulia chakula, manyani yake yalifanya vilevile. Kuona vile watumishi walidukuana, wakanongo'onezana kuwa labda bwana wao alipata wazimu.

Liwali wa Janibu alipenda unadhifu. Haikutazamiwa kuwa aliweza kukubali dhila ya kula na manyani mkono kwa mkono. Watumishi wote walikirihika, lakini Adili hakuwatazama kamwe. Aliendelea kula na manyani mpaka wote wakashiba.

Walipokwisha kula Adili alichukua kitambaa akajifuta mdomo. Manyani yalipewa vitambaa vyao yakajifuta pia. Watumishi wake walijizuia wasicheke lakini haikuwezekana, waliangua kicheko mbele ya bwana wao, "kwa-kwa-kwa!" Adili hakusema neno. Alijua kama mtu yeyote angeliona jambo kama lile asingaliweza kujizuia kucheka. Alipoondoka mezani na manyani yake, watumishi walichukua makombo wakayamwaga chini. Hawakuweza kula makombo ya manyani. Baada ya kumaliza kazi watumishi walipewa ruhusa kwenda zao, lakini hawakwenda kama ilivyokuwa desturi yao. Siku ile vitanda vitatu vya dhahabu vilitandikwa chumbani kwa Adili.

Watumishi walitaka kuona kama vile viwili vitalaliwa na manyani. Kwa hivi walipotoka nyumbani walijibanza nyuma ya madirisha wakachungulia ndani. Lahaula, walimuona Adili amelala chumba kimoja na manyani! Walipotosheka kuwa bwana wao alikuwa mwehu walikwenda zao na mioyo iliyoghadhabika.

# ARUSI

Adili alipolala, mtingisho mkubwa ulitokea chumbani mwake, sakafu ikapasuka. Kuzinduka uso wake ulikutana na uso wa Huria.

Wa kwanza ulijaa matumaini, na wa pili ulituna kwa hasira. Nyuso zao zilisomana. Kila uso ulijaribu kuzua mzungu wake.

Adili alivunja amri aliyopewa mara tatu. Alionekana amezoea kuhalifu. Kukomeshwa mazoea yake alipasa kugeuzwa nyani kama ndugu zake. Walakini, kabla ya hili kuwa Huria alitaka kusikia kama Adili alikuwa na udhuru wa kujitetea.

Adili hakusema, lakini tabasamu la mvuto mwingi inacheza usoni mwake. Alichukua barua ya Rai akampa Huria.

Huria aliposoma barua hakuweza kufanya alilokusudia. Alitoweka akaenda ujinini kumshauri baba yake. Barua ya Rai ilipowekwa mbele ya Kisasi, kuopolewa kwa ndugu zake Adili kuliidhiniwa. Huria alimwuliza mfalme wa majini labda haja ya mfalme wa wanadamu isingalikubalika ingalikuwaje.

Baba yake alieleza, mfalme wa wanadamu aliweza kufanya dhara aliyotaka kwa majini. Alikuwa mwanadamu, mwanadamu alikuwa bora kuliko jini. Majini katika Jua, Mwezi, Mushtara, Zebaki, Zuhura, Mirihi, Sumbla, Zohali, Sarateni, Kausi na Utaridi hayakuweza kushindana na watu katika ardhi.

Majini yaliweza kugeuza watu katika umbi lolote, lakini watu waliweza kufunga majini yote katika chupa moja. Magereza yao yalikuwa mabaya sana. Kama mtu asingalikuwa mzembe mwenyewe, busara ya jini ingalikuwa busara yake. Alipasa kuheshimiwa kama alitaradhia heshima yake.

Mara ile Huria alirudi kwa Adili akatangaza kuwa haja ya Rai ilifaulu. Mfalme wa majini alikubali ndugu zake kuwa watu tena.

Aliyabadili manyani akasema " tokeni katika uhayawani mrudi katika utu." Walikuwa watu tena, wakajiangusha miguuni mwa ndugu yao kuomba radhi. Adili alimshukuru Huria; na punde wakaagana.

Asubuhi watumishi walimuona bwana wao na watu wawili. Walitambua kuwa walikuwa ndugu zake. Walipouliza kuwa walikuwa wapi kwa muda mrefu bwana alijibu kuwa walikuwa manyani yaliyoonekana jana yakila naye. Walifurahi kumuona bwana wao sio kichaa, wakamuombea azidishiwe furaha katika maisha yake.

Baada ya kustaftahi, aliwavika ndugu zake nguo akapanda nao farasi kwenda Ughaibuni. Liwali Adili alipofika Ughaibu na habari kuwa manyani yake yalikuwa watu tena palikuwa na furaha kubwa sana. Jitihadi na kufaulu kwa Rai kuliandikwa katika kumbukumbu za dunia. Hasidi na Mwivu walipoletwa barazani kila mtu aliajabia sura zao, walikuwa wazuri ajabu.

Mfalme wa Ughaibu alimsifu Adili kuwa alikuwa sababu kubwa ya wokovu kwa ndugu zake katika dhima ya wanyama.

Mateso yaliyompata yalishinda uvumilivu wa mtu. Alivumilia mateso mengi kwa ajili yao. Alikuwa mwanamume barabara na fahari ya Ughaibu. Nchi yake ilimsifu hivi, haijulikani nchi yangu au yako ingalimsifiaje mtu wa namna ile.

Alipogeuka kwa ndugu zake Adili, Rai alionya; kama wavivu wajitahidi kuwa hodari, ilikuwa kinyume cha hodari kuwa mvivu; kama waovu walitakiwa kuwa wema, ilichukiza wema kuwa wovu; kama masikini walitafuta utajiri, ilikuwa ujinga matajiri kufuja walichokuwa nacho; kama mbegu kidogo iliongezwa mchanga, ilikuwa uharabu mtu kuua ndugu yake; pia ilikuwa aibu kubwa sana kwa wazuri kutenda uovu.

Wakamilifu walikuwa na nafasi kubwa duniani kuliko wapungufu. Maonyo ya mfalme yalikuwa mwanana, lakini yalishinda mioyo ya watu waliokusudiwa kuonywa.

Walimshukuru, wakaahidi kuwa walikoma kutenda dhara kwa ndugu yao, na kwa kitu chochote kilichokuwa na maisha. Ahadi hii haikuvunjwa.

*“Mawe huwa dhahabu*
*johari na chuma,*
*Na mtu anapotubu"*

*Dhambi yake kukoma,*
*Nishani zake thawabu*
*Na heshima ya daima.*

Adili alipanda farasi akarudi Janibu na ndugu zake. Njiani alikutana na mabibi watatu waliopanda farasi vilevile.

Mabibi wenyewe walikuwa wazuri na watanashati sana. Wa kwanza alikuwa Mwelekevu aliyeokolewa na Mrefu. Macho ya Adili na ya Mwelekevu yalipokutana mioyo ya giza ilijaa nuru tena. Wote wawili walishuka chini wakaamkiana.

Aha, ilikuwa furaha kubwa ilioje! Mioyo miwili ya mapenzi iliyopoteana ilikutana tena. Neno halikuwezekana kusemeka. Walitazamana, wakachekana. Walishikana mikono, wakabusiana. Walikuwa katika siku bora ya maisha yao.

Adili alipomwambia Mwelekevu kuwa wavulana wawili warembo aliokuwa nao walikuwa ndugu zake, Mwelekevu kadhalika alisema kuwa wasichana wawili watanashati aliofuatana nao walikuwa marafiki zake.

Watu wote wanne walishuka chini wakaamkiana vilevile. Kisha wote walipanda farasi wao wakashika njia mpaka Janibu

Walipofika palifanywa arusi tatu siku moja. Siku hiyo ilikuwa kubwa kuliko yoyote iliyopita Janibu.

TAMATI